# Nipashe

Jumamosi Aprili 11, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580203

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




## Diwani jela miaka 20 kwa kuhujumu uchumi mil. 4/-

UKURASA 3




UKURASA 11

# Makanisa yafanya mabadiliko Pasaka

• **Ni** ya Ibada, lengo ni kufuata mwongozo kuepusha maambukizi corona... *Endelea ukurasa 2*



Waumini wa Kikristo wakiwa wamekaa kwa kuachiana nafasi kubwa ili kuchukua tahadhari ya maambukizi ya virusi vya corona, wakati wa Ibada ya Ijumaa Kuu kwenye Kanisa Katoliki Parokia ya Mtakatifu Maximilian Maria Kolbe la Mwenge, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



### BAA LA CORONA

**Unaweza kupata maambukizi ya virusi kama uko ndani ya mita moja kutoka kwa mtu mwenye Covid -19, au kwa kushika sehemu isiyosafishwa na kugusa macho, pua au mdomo kabla ya kunawa mikono. WHO**

- **Epuka mikusanyiko ya watu**
- **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
- **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
- **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**

## CAG abaini kasi kubwa ya uvamizi Mgodi wa Tanzanite

UKURASA 5

## Saba wapya wathibitishwa kuwa na virusi vya corona

UK.3





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



**MICHEZO** **SILAHA MPYA KUTUA YANGA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# CAG aona shida kwa uuzaji rejareja wa gesi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amesema amebaini kuwapo kwa udhibiti usioridhisha kwenye uuzaji rejareja wa gesi (Liquified Petroleum Gas).

Katika ripoti yake ya ukaguzi wa mashirika ya umma kwa mwaka wa fedha 2018/19 iliyowasilishwa bungeni jijini hapa Jumatatu, CAG Charles Kichere, anasema kuwa kwa mujibu wa Kanuni za Gesi za Mwaka 2018, Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (Ewura) ni msimamizi wa shughuli zinazohusu gesi kwenye mitungi kwa wasambazaji, wauzaji wa jumla, na wauzaji wa rejareja.

Anasema kuwa, kwa mujibu wa Kanuni ya 10(2) ya Kanuni za Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji, mamlaka inatakiwa kutoa leseni kwa wauzaji na wasambazaji wa gesi iliyosindikwa na kujazwa kwenye mitungi, lakini kanuni haiwataji wauzaji wa rejareja wa gesi. CAG anasema hali hiyo inatengeneza mwanya wa kushindwa kusimamia wauzaji wa rejareja na hivyo kuwa na hatari ya usalama, ubora na viwango vya gesi inayouzwa kwa wateja wa mwisho.

"Vilevile, nilibaini kuwa mamlaka haisimamii bei ya gesi iliyosindikwa kwa mujibu wa Kifungu cha 7(b)-iv cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji ya Mwaka 2001 ambayo inaitaja mamlaka kuwa msimamizi wa viwango vya bei na tozo kwa nishati na maji.

"Bei za soko zinakuwa na udhibiti kwa wauzaji wa jumla wa gesi iliyosindikwa. Mamlaka ilieleza kuwa haina uwezo wa kusimamia kwa sasa ikisubiri kuanza kwa mfumo wa uagizaji wa pamoja wa gesi (Bulk procurement system) unaosubiri ujenzi wa miundombinu katika Bandari ya Dar es Salaam kwa ajili ya kupokea gesi. Sababu nyingine ni kukosekana kwa mfumo wa taarifa sahihi za shehena ya gesi inayoagizwa toka nje ya nchi," anabainisha.

CAG anapendekeza Menejimenti ya Mamlaka ifanye mapitio ya kanuni zake za gesi iliyosindikwa za mwaka 2018 ili kuhakikisha zinawahusisha wauzaji wa rejareja ili kuongeza usimamizi wao na kuharakisha kuanzisha mfumo wa uagizaji wa pamoja wa gesi iliyosindikwa na mfumo wa taarifa kuiwezesha mamlaka kupanga na kusimamia bei za gesi.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akizungumza na Balozi wa Jamhuri ya Watu wa China nchini, Wang Ke, ofisini kwake, eneo la Mlimwa, jijini Dodoma, jana. **PICHA: OWM**

# Makanisa yabadili utaratibu ibada Pasaka

**Na Waandishi Wetu**

MAKANISA mbalimbali nchini, yamefanya mabadiliko ya utaratibu wa kuendesha ibada na misa za Ijumaa Kuu na Pasaka katika kukabiliana na homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya Corona (Covid-19).

Mabadiliko hayo ni mwongozo wa idadi ya watu wa kuhudhuria mazishi na sherehe za ubatizo na ndoa.

Wakizungumza na Nipashe jana kwa nyakati tofauti, viongozi wa madhehebu ya dini mbalimbali, walieleza walivyojizatiti kuhakikisha hakutokei maambukizi ya ugonjwa huo wakati wa Sikukuu ya Pasaka na baada.

Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kirutheri (KKKT), Dk. Fredrick Shoo, akizungumza na Nipashe, alisema tangu kutangazwa kwa ugonjwa huo, KKKT ilitoa mwongozo wa ibada zitakavyokuwa zinafanyika.

"Hata hapa Moshi na maeneo mengine hatua ambazo zimeshachukuliwa tumewaelekeza wachungaji wetu na waumini tahadhari ambazo serikali imezitoa ikiwa ni pamoja na kupunguza idadi ya watu na kuongeza ibada.

"Tumeongeza ibada kulingana na kanisa lenyewe, wale wenye ibada moja wanaongeza ya pili, wenye ibada mbili zimeongezeka hadi tatu."

Kadhalika, alisema wanazingatia utaratibu wa kukaa mbali mtu na mtu na kunawa mikono kama ilivyoagizwa na serikali pamoja na usafi wa vifaa vya kanisa kabla na baada ya ibada.

"Pasaka, tutakuwa na ibada ya asubuhi na ya mchana, tumeelekeza kuweka hema nje ya kanisa ili waumini wasikaribiane," alisema.

Kuhusu ndoa na ubatizo, Dk. Shoo alisema wameweka utaratibu kwamba zenye ulazima pekee ndiyo zifungwe katika kipindi hiki kwa masharti ya watakaokwenda kanisani, maharusi, washenga na wazazi wa pande mbili.

Vile vile, alisema baada ya ubatizo au ndoa wamewataka waumini kusiwe na sababu ya kufanya sherehe ambazo zitasababisha mkusanyiko wa watu.

"Tumetoa maelekezo ya jumla baadhi ya huduma kama ndoa na ubatizo kusogezwa, isipowezekana idadi ya watu ipungue wawe watu wa karibu na wahusika," alisema.

Akizungumzia ibada za mazishi, Dk. Shoo alisema wameweka utaratibu kuwa wanaotakiwa kuhudhuria wasizidi watu 50.

Kwa mujibu wa ujumbe wa Pasaka kwa waumini wa Katoliki uliotolewa na kanisa hilo, umesisitiza mambo makubwa mawili likiwamo virusi vya corona.

**KANISA KATOLIKI**

Akitoa taarifa hiyo kwa niaba ya kanisa, Askofu wa Jimbo la Mburu, Padri Anthony Legwen, alisema kanisa linawataka waumini wote kuungana kumuomba Mungu awaondoe kwenye janga hilo.

"Pengine tunajiuliza msaada wetu utatoka wapi? Msaada wetu utatoka kwa Mungu tu, Zaburi 121:1-2, yeye aliumba mbingu na dunia, ni yeye tu anaweza kuondoa tishio hili na kuturudishia amani."

"Tuzingatie pia maelekezo yote yanayotolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO), serikali na wadau wote wenye nia njema kama tahadhari kujikinga na maambukizi ya virusi hivyo."

Naye, Askofu Tarcisius Ngalalekumtwa wa Jimbo Katoliki Iringa, alisema wanachokifanya ni kufuata mwongozo wa serikali kwa kanisa kwa kuzingatia kutokuwa na mikusanyiko na usafi.

**KANISA ANGLIKANA**

Padri Msaidizi, Patrick Challo, wa Kanisa la Anglikana, Kristo Mfalme Kinondoni, alisema wamezingatia miongozo ya serikali iliyotoa na pia kufupisha baadhi ya vitu katika ibada ili waumini wasikae muda mrefu.

"Ushirika Mtakatifu meza ya Bwana badala ya kumlisha muumini moja kwa moja mdomoni, anapewa mkononi baada ya kunawa mikono.

"Matukio ya ndoa tumewaambia ikiwa ni lazima wanaweza kufunga mwezi huu kinyume na hapo hatushauri. Tangu ugonjwa huu utangazwe kanisa letu la Kinondoni hatujafungisha ndoa, msiba ukitokea tunaomba waje wachache kanisani."

Alisema katika mkesha wa Pasaka watakuwa na ubatizo, lakini kwa utaratibu mpya ambao wazazi watalazimika kununua mshumaa na kitambaa maalumu cha kumfunika anayebatizwa badala ya vifaa hivyo kutoka kanisani.

Kwa upande wake, mtume na Nabii, Boniface Mwamposa, alisema kanisa lake limechukua tahadhari ya kukaa umbali wa mita moja kati ya mtu na mtu na wapo kwenye maombi ya kufunga kwa siku tatu.

Kwa upande wake, Mchungaji Staley Nnko, kutoka Kanisa la Mlima Moto, walianza juzi kwa maombi ya siku tatu.

Waumini wapeana nafasi

Katika Ibada ya Ijumaa Kuu, baadhi ya makanisa yalianza kuendesha ibada zao kwa kupunguza idadi ya watu kanisani.

Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Azania Front jana iliendesha ibada yake na waumini wachache waliokuwa wamekaa umbali wa mkono kwa mkono ulioelekezwa na serikali.

Askofu wa Dayosisi hiyo, Dk. Alex Malasusa, aliyekuwa akiongoza ibada hiyo, aliwaambia waumini wapungiane mikono badala ya kushikana.

Akihubiri katika ibada hiyo, Askofu Malasusa alisema ni vyema watu wakaendelea kumwamini na kumtegemea Mungu katika kila jambo.

Alisema watu wengi wameacha kumtegemea Mungu na badala yake wanahangaika kufanya mambo ya kuwafurahisha binadamu na hivyo kujikuta wakiingia kwenye mkumbo wa kutenda maovu.

**ASKOFU NTIRUKA ASISITIZA**

Askofu mstaafu wa Kanisa la Aglikana Tanzania, Dayosisi ya Tabora Francis Ntiruka, amewataka waumini wa dini ya Kikrito nchini kuendelea kuzingatia maelekezo yanayotolewa na wataalam wa afya katika kujikinga na corona msimu huu wa Pasaka.

Katika mahubiri yake ya ibada ya Ijumaa kuu iliyofanyika katika kanisa kuu Aglikana la roho mtakatifu jijini hapo, alisema Ijumaa kuu ni siku yenye huzuni kwa Wakristo duniani ambayo pia imeambatana na janga la ugonjwa wa corona ambalo ni tishio katika maeneo mbalimbali.

"Ugonjwa huu umepoteza watu wengi sana duniani wengi wamepoteza ndugu zao jamaa zao pamoja na marafiki wao wa karibu hivyo basi ndugu zangu wakati tunaendelea kufanya maombi, lakini pia tuhakikishe kuwa tunazingatia maelekezo ya wataalamu wetu wa afya bila kupuuza," alisema Askofu Ntiruka.

Alisema, wanatakiwa kuendelea kufanya maombi ili Mungu asaidie kuondoa janga hilo linaloitesa dunia.

Akizungumzia ibada ya Ijumaa Kuu alisema, waumini wa dini hiyo wanatakiwa kuondoa dhana ya kuwa kifo cha Yesu Kristo kilikuwa cha ajali au bahati mbaya.

"Kifo cha Kristo ndugu zangu haikuwa bahati mbaya ni shauri ya Mungu kwa kuwa kilitokea ili kutuondolea laana, hukumu na adhabu ya dhambi hivyo kutokana na hali hiyo sisi ni watoto tulio huru,"alisema.

■ **Imeandikwa na Romana Mallya, Elizabeth Zaya (Dar) na Paul Mabeja (Dodoma)**

## HABARI KITAIFA



Viongozi wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), ngazi ya wilaya ya Dodoma Mjini, wakimuomba Mungu ili kuliepusha taifa na ugonjwa wa corona katika dua iliyofanyika kwenye ukumbi wa Shule ya Sekondari ya Jamhuri ya wilayani humo, jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# CAG: Mauzo mazao nje ya nchi yamepungua

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), amebaini kupungua kwa mauzo ya mazao nje ya nchi na kushuka kwa kiwango na bei za mazao hayo.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2018/19, iliyowasilishwa bungeni jijini hapa Jumatatu, CAG Charles Kichere, anatahadharisha kuwa hali hiyo ikiendelea itawakatisha tamaa wakulima na kuhatarisha uchumi wa nchi.

Anasema kilimo kinachangia sehemu kubwa ya kipato na kupunguza umaskini kwa watu wanaoishi vijijini na kwamba Mpango-Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (Mkukuta) - II, 2010, umeainisha dosari zinazoikabili sekta ya kilimo kuwa ni kukosekana kwa huduma za kutosha za ugani, masoko yasiyo na uhakika na ushindani katika bei, namna isiyofaa ya kuwekeza katika kilimo na miundombinu mibovu ya kusaidia shughuli za kilimo.

CAG anabainisha kuwa, tangu uhuru, serikali imekuwa ikisaidia sekta ya kilimo ikihusisha pia kuanzisha taasisi mbalimbali za kilimo ambazo zimepewa mamlaka ya kutekeleza majukumu ambayo yanaweza kupunguza dosari zilizotajwa katika Mkukuta II. Anazitaja taasisi hizo kuwa ni pamoja na Bodi ya Sukari Tanzania (SBT), Bodi ya Chai Tanzania (TBT), Bodi ya Korosho Tanzania (CBT), Bodi ya Tumbaku Tanzania (TTB), Bodi ya Mkonge Tanzania (TSB), Bodi ya Kahawa (TCB), na Bodi ya Mazao Mchanganyiko (TCBP).

Zingine ni Taasisi za Utafiti wa Kilimo kama vile Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania (TaCRI) na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TaLIRI) na mifuko ya maendeleo ya mazao kama vile Mfuko wa Kahawa, Mfuko wa Korosho, na Mfuko wa Pamba ambayo hivi karibuni ulivunjwa na majukumu yake kuhamishiwa kwenye bodi za mazao husika.

"Hata hivyo, pamoja na kuundwa kwa taasisi hizi, bado kuna changamoto (vikwazo) zinazozikumba taasisi na bodi hizi ikiwa pamoja na mwingiliano wa majukumu ya taasisi hizi (kama shughuli za ugani na kutangaza mazao hayo); kiwango cha fedha kisichotosheleza shughuli za taasisi hizo; na upungufu katika kulinda ubora wa mazao na kupelekea mazao hayo kukosa sifa za kuuzika kwa bei kubwa sokoni," anasema.

CAG anasema Sheria ya Tumbaku Na. 24 ya Mwaka 2001 na Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mazao Na. 20 ya Mwaka 2009 na Sheria ya Chai Na. 3 ya Mwaka 1997, zinazipa bodi za mazao jukumu la kuishauri serikali juu ya sera na mikakati ya kuendeleza, kuyasimamia na kulinda ubora wa mazao hayo.

Anabainisha kuwa takwimu zinaonyesha mwenendo wa uzalishaji wa tumbaku kwa miaka mitano kwa ujumla ulishuka kutoka tani 71,999 mwaka 2014/2015 hadi tani 60,691 mwaka 2018/2019.

Anasema mwendelezo wa kushuka kwa uzalishaji wa tumbaku ulitokana na sababu nyingi ikiwamo kupungua kwa mahitaji ya tumbaku katika soko la dunia kulikosababishwa na kampeni za kupinga matumizi ya tumbaku zilizofanywa na Shirika la Afya Duniani (WHO) na kuingizwa kwa sigara za kieletroniki.

CAG anabainisha kuwa, daraja la juu la tumbaku pia lilishuka kwa tani 7.23 kwa mwaka 2018/2019 kulinganishwa na mwaka 2017/2018. Pia, pato la tumbaku iliyouzwa nje lilipungua kutoka Dola za Marekani 132,611,000 mwaka 2017/2018 hadi Dola za Marekani 92,927,000 mwaka 2018/2019.

# Saba wapya wathibitishwa kuwa na virusi corona

**Na Elizabeth Zaya**

TANZANIA imebaini visa vipya saba vya ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona (Covid -19) na kufanya idadi ya wagonjwa kufikia 32.

Watu wawili waliokuwa na ugonjwa huo wamefariki, mmoja jana usiku na mwingine alfajiri ya kuamkia jana wakati wakipatiwa matibabu, huku watano wakipona na kuruhusiwa kutoka hospitalini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari jijini Dar es Salaam na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, wagonjwa watano wote ni Watanzania na wakazi wa Mkoa wa Dar es Salaam.

Katika taarifa hiyo, alisema wagonjwa wanne ni wanaume wenye umri wa miaka 68, 57, 54, 41 na mwanamke mmoja mwenye umri wa miaka 35. "Hivyo sasa jumla ya watu waliothibitishwa kupata maambukizi ya Covid-19 nchini ni 32, kati ya hawa watano wamepona na wengine 24 wanaendelea vizuri na matibabu,"alisema Ummy katika taarifa yake.

"Pia tunasikitika kutoa taarifa ya vifo viwili vilivyotokea leo (jana) miongoni mwa wagonjwa waliothibitishwa kuwa na maambukizi ya corona, hivyo kufanya idadi ya vifo kufikia vitatu tangu ugonjwa huu uliporipotiwa nchini," alisema Ummy.

Alisema waliofariki ni wanaume wawili Watanzania na wakazi wa Dar es Salaam wote, mmoja akiwa na umri wa miaka 51 waliyemtolea taarifa Aprili 8, mwaka huu, pamoja na mwingine wa miaka 57 aliyetolewa taarifa jana.

"Kwa mara nyingine serikali inaendelea kuwasisitiza wananchi kuchukua tahadhari ya kujikinga na ugonjwa huu kama tunavyowapatia taarifa na elimu mara kwa mara kupitia njia mbalimbali,"alisema Ummy.

# Diwani jela miaka 20 kwa kuhujumu uchumi mil. 4/-

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Dodoma, imewahukumu kifungo cha miaka 20 kila mmoja aliyekuwa Diwani wa Kata ya Mvumi Makulu, wilayani Chamwino mkoani Dodoma, Kedmond Sungura na fundi Augustine Mwimbe, kwa kosa la kuisababishia serikali hasara ya Sh. milioni nne.

Mbali na hukumu hiyo pia watuhumiwa hao wametaifishiwa mali zao ikiwa ni moja ya adhabu ya makosa yanayowakabili. Hukumu hiyo imetolewa juzi katika mahakama hiyo baada ya Hakimu Mayumba kujiridhisha na ushahidi uliotolewa mahakamani hapo. Washtakiwa walisomewa kosa moja la kusababisha hasara ya Sh. milioni nne kwa kutumia vibaya fedha hizo zikiwa ni sehemu ya Sh. 6,500,000 zilizotolewa na Mfadhili Father John Norman wa ofisi ya Amani Development Organization, iliyopo katika kijiji cha Makang'wa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la wodi kwenye zahanati ya Mvumi Makulu.

Uchunguzi wa Takukuru ulionyesha kwamba, utaratibu wa matumizi ya fedha hizo haukuzingatiwa na ujenzi uliofanyika, haukukidhi viwango na hivyo ukasimamishwa na halmashauri ya Chamwino.

Katika kesi hiyo washtakiwa wengine watatu wameachiwa huru kutokana na kutokuwa na hati yoyote katika kesi hiyo.

Washtakiwa walioachiwa huru ni Judith Maninje, Oscar Ngoma na Yubeth Mhawi, ambao hawakukutwa na hatia katika kesi hiyo.

Kesi hiyo imeendeshwa kwa miaka miwili na hukumu hiyo imetolewa ili kuwa fundisho kwa wengine wasifanye makosa ya aina hiyo ya uhujumu uchumi ambao unaisababishia serikali hasara ya upotevu wa mali na pesa.

# Mabasi ya Mwendokasi yalivyonunuliwa kifisadi-2

**KATIKA toleo la jana tulieleza jinsi ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) mwaka wa fedha 2018/19, ilivyobaini ufisadi katika ununuzi wa mabasi, vipuli na usimamizi wa mali za kudumu kwenye Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka, maarufu mwendokasi. Sehemu ya pili na ya mwisho inaendelea kubainisha madudu zaidi.**

**MALIPO BILA MKATABA**

Katika ripoti yake hiyo, Kichere anaendelea kubainisha kuwa Kipengele cha 6.1 cha mkataba wa mtoa huduma ya mpito baina ya DART, UDART na Shirika la UDA uliotiwa saini Aprili 24, 2015, kinataka mapema iwezekanavyo baada ya kuingiwa kwa mkataba huo, DART na UDART kwa pamoja watapaswa kuiteua Benki ya NMB kama msimamizi na mtunzaji wa fedha (Fund Manager).

Anasema kupitia mahojiano yake na uongozi wa NMB na Kampuni ya UDART, ilibainika kuwa hakukuwa na makubaliano ya kuichagua NMB kuwa msimamizi wa fedha.

"Hata hivyo, kupitia taarifa ya mgawanyo wa mapato yanayofanywa na Benki ya NMB kutoka katika Akaunti Na. 20110021252 DART INTERIM SER FARES COLL ACC kwa kipindi cha miaka mitatu na miezi minane kuanzia Mei 16, 2016 hadi Januari 22, 2020, ilibainika kuwa jumla ya Sh. bilioni 1.78 kilitozwa na NMB kama gharama za usimamizi na utunzaji wa fedha bila makubaliano.

"Pia wabia (UDA na UDART) walisaini mkataba na NMB Machi 25, 2019 wa usimamizi wa fedha za mradi. Kampuni ya Simon Media Group ilipewa mkataba wa kufanya usafi kwenye mabasi na vituo vya mabasi ya mwendokasi kwa kipindi cha kuanzia Mei 6, 2016 hadi Aprili 29, 2017.

"Hata hivyo, ukaguzi wangu ulibaini kuwa kampuni iliendelea kutoa huduma licha ya mkataba wake kwisha Aprili 29, 2017 na jumla ya Sh. milioni 698.54 zilipwa hadi kufikia Januari 2020.

"Vilevile, kuanzia Novemba 22, 2016 hadi Mei 3, 2018, Kampuni ya UDART ililipa Kampuni ya Simon Media Group jumla ya Sh. bilioni 1.01 kama ujira wa matangazo (advertisement commission). Hata hivyo, hakukuwa na mkataba baina ya Kampuni ya UDART na Kampuni ya Simon Media Ltd juu huduma ya matangazo.

"Malipo yaliyofanywa bila uwapo wa mikataba hayakustahili kulipwa kwa kampuni husika. Hivyo, ninashauri UDART na watoa huduma kuingia mikataba kwa kufuata sheria na miongozo ya ununuzi na kutathmini uhalali wa malipo yaliyofanywa bila mikataba," anasema.



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, CAG Charles Kichere.

**UTATA UNUNUZI HISA**

CAG pia anasema ukaguzi wake kwenye ununuzi wa hisa za UDA na Kampuni ya Simon Group Limited, ulibaini Kampuni ya Simon Group Limited ilitumia mali za UDA kujipatia mkopo na kuitumia Kampuni ya UDART kulipia mkopo ambao ndiyo ulitumika kununulia hisa katika Kampuni ya UDA.

Anafafanua kuwa, mnamo Septemba 25, 2013, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam iliingia mkataba na Kampuni ya Simon Group Ltd wa mauzo ya hisa milioni 3.63 kwa bei ya Sh. 1,618 kwa hisa, jumla ya Sh. bilioni 5.87 zilipaswa kulipwa.

Kutokana na kutiwa saini kwa mkataba huo, Kampuni ya Simon Group Limited ilipewa haki ya kutumia mali za Kampuni ya UDA, na ili kulipa gharama ya hisa hizo, Kampuni ya Simon Group Ltd ilichukua mikopo miwili toka NMB Julai 9, 2015 na Machi 31, 2016 kwa lengo la kulipia gharama za ununuzi ya hisa kwa kuweka dhamana ya mikopo mali za Kampuni ya UDA.

"Kampuni ya Simon Group Ltd ilishindwa kufanya marejesho ya mikopo na hadi kufikia Agosti 22, 2017, deni la mkopo lilifikia Sh. bilioni 6.93 kutokana na kukua kwa riba.

"Mwenyekiti Mtendaji na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya UDART kwa vipindi tofauti waliuagiza uongozi wa Kampuni ya UDART kufanya malipo ya mkopo huo kwenda NMB.

"Ukaguzi wangu ulibaini kuwa hadi kufikia Januari 31, 2019, Kampuni ya UDART ilikuwa imefanya jumla ya malipo ya Sh. bilioni 4.75 ambazo zinajumuisha Sh. milioni 295 zilizolipwa katika akaunti ya benki yenye namba 20406600306 ya Kampuni ya Simon Group Ltd toka akaunti ya benki ya Kampuni UDART yenye namba 20110017639, na kiasi cha Sh. bilioni 4.46 kililipwa toka akaunti ya benki ya UDART yenye namba 20110028055 kwenda akaunti ya benki ya Kampuni ya Simon Logistics Group Ltd yenye namba 20110017722.

"Kampuni ya Simon Group Ltd ilinunua hisa za UDA na kufanya malipo ya mkopo kwa kutumia njia za udanganyifu. Hivyo, ninapendekeza kuwa serikali ifute hisa za Simon Group Ltd kwa kuwa zilipatikana kwa njia za udanganyifu; na hatua stahiki za kisheria zichukuliwe kwa Mwenyekiti Mtendaji na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya UDART kwa kuwezesha ubadhilifu huu kutokea," CAG anashauri.

**USIMAMIZI MBOVU**

Kichere pia anabainisha kuwa mnamo Oktoba Mosi, 2011, Kampuni ya Simon Group Ltd iliingia mkataba na Shirika la UDA kwa ajili ya ukodishaji wa viwanja vitatu vyenye ukubwa wa jumla ya ekari 13.6 kwa gharama ya Sh. milioni 400 kwa mwaka kwa muda wa miaka 10 kuanzia Juni Mosi 2012 hadi Mei 30, 2022.

Hata hivyo, anasema uchunguzi wake ulibaini kuwa kupitia hesabu za UDA kuanzia tarehe Juni Mosi, 2012 hadi Desemba 31, 2019, malipo ya kodi hayakufanyika ambayo ni sawa na Sh. bilioni 3.44 kwa kipindi cha miaka minane na miezi sita.

"Vilevile, ilibainika kuwa Kampuni ya UDA haikuchukua hatua stahiki kuhakikisha kuwa Kampuni ya Simon Group Limited inafanya malipo husika.

"Pia, nilibaini Kampuni za Simon Logistic Group Ltd na Simon Group Ltd ambazo ni kampuni wabia, zilikodisha kitalu namba 36 kilichoko Kurasini jijini Dar es Salaam kinachomilikiwa na Kampuni ya UDA kwa kampuni za Tanzania Breweries Limited (TBL), OLAM Tanzania Ltd, Tanzania Distilleries Limited (TDL) na CMA CGM.

"Kampuni hizo zililipa kiasi cha Sh. bilioni 14.08 na Dola za Marekani milioni 1.13 kama kodi ya pango. Hata hivyo, niligundua kuwa Kampuni ya Simon Logistic Group Ltd iliyokodisha kampuni hizo haikuwa na mkataba wa ukodishaji toka kwa mmiliki wa eneo ambaye ni Kampuni ya UDA.

"Aidha, ingawa ilipokea malipo ya ukodishaji toka kwa kampuni zilizotajwa, Kampuni ya Simon Group Ltd haikuilipa Kampuni ya UDA. Kampuni ya UDA haikunufaika na ukodishaji wa viwanja vyake na badala yake ni Kampuni ya Simon Group Ltd ndiyo iliyonufaika.

"Hata hivyo, Menejimenti ya Kampuni ya UDA haikuchukua hatua stahiki kuhakikisha kuwa Kampuni ya UDA inanufaika na ukodishaji wa mali zake. Ninapendekeza Menejimenti ya Kampuni ya UDA ichukue hatua stahiki kuhakikisha inalipwa kodi ya ukodishaji toka Kampuni ya Simon Group Ltd na Simon Logistic Group Ltd," anashauri.

**BIL. 6.56/- ZA TEHAMA**

Vilevile, CAG anasema ili kuboresha utolewaji wa huduma katika Mradi wa Mabasi ya Mwedokasi, Oktoba 19, 2015 Kampuni ya UDART iliingia mkataba na Kampuni ya Kapsch CarrierCom Belgium NV (KCC) kwa ajili ya ununuzi na usimikaji wa vifaa vya mfumo wa ITS kwa gharama ya Euro milioni 3.4, sawa na Sh. bilioni 8.55 (Euro 1=Sh. 2,509).

Anasema Mfumo wa kieletroniki wa huduma za usafiri (ITS) ulianza kutumika rasmi Mei 2016 baada ya kukamilika kwa usimikaji wake, huku jumla ya malipo yaliyokuwa yamefanyika kwa mkandarasi yakifikia Sh. bilioni 6.56.

Hata hivyo, CAG anasema kuanzia Juni 18, 2018, Kampuni ya UDART iliacha kutumia mfumo huo na kuhamia kwenye utumiaji wa mfumo wa kieletroniki wa makusanyo ya mapato ya mamlaka za serikali za mitaa (LGRCIS) kukusanyia mapato kwa kipindi ambacho mchakato wa kutengeneza mfumo mpya ulikuwa unaendelea. "Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni UDART alieleza kuwa, mfumo huo uliachwa kutumiwa kutokana na kuwa vifaa vilivyofungwa havikuwa wazi kwa mfumo mwingine wowote. Hata hivyo, Mkurugenzi wa Maxcom Africa Ltd alipingana na hoja hiyo na kueleza kuwa Mfumo wa ITS unaweza kutumika kwenye mifumo mingine, kwa mfano, mfumo huo uliunganishwa na mifumo ya benki na simu (Integration with Banks and Mobile Money Platform).

"Uwekezaji uliofanywa na UDART kwenye utengenezaji wa mfumo wa ITS ulitumia gharama kubwa. Hivyo, kwa kutotumika kunasababisha kukosekana kwa tija ya uwekezaji huo; pia kama utabadilishwa, serikali itakuwa imepata hasara ya uwekezaji.

"Ninapendekeza UDART pamoja na mkandarasi wazifanyie kazi changamoto (dosari) za mfumo wa kieletroniki wa ITS ili uendelee kutumika badala ya kuwekeza kwenye utengenezaji wa mfumo mpya wa Tehama," CAG anashauri.

HABARI KITAIFA

# Majaliwa, Balozi China wajadili corona

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amekutana na Balozi wa China nchini, Wang Ke, na kujadiliana masuala kadhaa kuhusiana na virusi vya corona (COVID-19).

Majaliwa ameishukuru Serikali ya nchi hiyo kwa misaada ambayo imetoa katika kukabiliana na ugonjwa wa homa ya mapafu unaotokana na maambukizi ya virusi vya corona (COVID-19).

"Tunaishukuru Serikali ya China kwa misaada ambayo imetupatia hadi sasa vikiwamo dawa na vifaa tiba. Na leo umesema kwamba kuna asasi za kiraia na wafanyabiashara wanakusanya vifaa vingine ili viletwe nchini vitusaidie kuzuia maambukizi, tunawashukuru sana."

Alitoa shukrani hizo jana ofisini kwake Mlimwa, jijini Dodoma, alipokutana na Balozi huyo. "Mchango wenu ni muhimu sana kwetu, kwa sababu tunaanza kupata uzoefu wa namna ya kupambana na ugonjwa huu," alisema.

Alisema Tanzania Bara na Zanzibar zinapata wagonjwa kwa sababu ni vituo vya biashara, lakini wageni wote wanaoingia nchini kwa sasa wanawekwa sehemu maalumu ambako wanapatiwa huduma zote wakiwa huko huko.

"Tunashukuru Watanzania wa pande zote mbili wanaendelea kupokea maelekezo wanayopewa, wanaendelea kujikinga na kuchukua tahadhari za kutozunguka ovyo ili wasisambaze maambukizi," alisema.

Alimshukuru Balozi huyo kwa niaba ya Serikali ya nchi hiyo kwa jinsi ambavyo waliwahudumia wanafunzi wa Kitanzania zaidi ya 500 wanaosoma China katika kipindi chote cha kupambana na ugonjwa huo.

Alisema Balozi wa Tanzania nchini China, Mbelwa Kairuki, amekuwa akileta taarifa za mara kwa mara kuhusiana na jinsi China ilivyowasaidia wanafunzi walioko huko na kuhakikisha wanakuwa salama.

"Leo hii Tanzania tumeanza kupitia tatizo lile lile ambalo liliwapata ninyi. Tuna wagonjwa wachache, lakini tuna kundi kubwa la wale waliokutana na wagonjwa na tunaendelea kuwafuatilia na kuwapima kila siku."

"Tunaendelea na jitihada za kuzuia maambukizi mapya, tunatoa elimu kwa wananchi wetu na kuwaelimisha kuhusu kunawa mikono na kutumia vitakasa mikono. Tunaendelea kufanya tathmini kila siku ya watu wanaopimwa. Tumezuia mikutano na mikusanyiko yote, tumefunga shule na vyuo, tumezuia michezo ili tusisambaze maambukizi."

Waziri Mkuu alimweleza Balozi huyo kwamba kwa sasa Tanzania imefunga mipaka yake kwa sababu hata nchi jirani zimefunga mipaka yao na endapo kuna wageni wanaingia nchini, ni lazima waende kwenye isolation centres ambako wanalazimika kukaa kwa siku 14.

Balozi Wang Ke alimfikishia salamu za shukrani Waziri Mkuu kutoka kwa Waziri Mkuu wa China, Li Keqiang.

Alimweleza Majaliwa kwamba nchi yake kwa sasa haina maambukizi, na kwamba wamelenga kuzuia maambukizi mapya kutoka nje ya nchi yasiingie nchini mwao.

"Kwenye baadhi ya miji tumefungua viwanda na vimeshaanza uzalishaji wa bidhaa ili kufufua uchumi wetu. Mwaka huu ni muhimu sana kwetu kwa sababu nchi yetu ilijipangia kuwa uwe ni mwaka wa kuhakikisha kuwa hakuna kabisa umasikini. Kwa hiyo, tunapambana kurejesha shughuli za kiuchumi zilizoathirika kutokana na ugonjwa huu," alisema.

Balozi Wang Ke alisema nchi yake imechagua baadhi ya nchi za Afrika ambazo inazisaidia kwa kubadilishana nazo uzoefu kupitia mikutano kwa njia ya video ili ziweze kukabiliana na ugonjwa huo.

"Zaidi ya hayo, kuna misaada ya vifaa tiba kwa ajili ya Serikali ya Zanzibar na Tanzania Bara, ambayo inakusanywa na asasi za kiraia na wafanyabiashara. Hii iko njiani, na ile ya Tanzania Bara itawasili wiki ijayo."



Mbunge wa Kilolo, mkoani Iringa, Venance Mwamoto (kushoto) akiwa na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), wilaya ya Kilolo, Yohanes Sarufu na viongozi wengine, wakikagua daraja lililosombwa na mafuriko eneo la Ilula juzi. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# CAG: Uvamizi Mgodi wa Tanzanite umeongezeka

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

LICHA ya hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali kuimarisha ulinzi katika mgodi wa madini ya Tanzanite mkoani Manyara, ikiwamo kujenga ukuta mrefu kuzunguka eneo lote la mgodi, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG), amebaini kuongezeka kwa uvamizi kwenye mgodi huo.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2018/19, CAG Charles Kichere, anasema amebaini kuongezeka kwa uvamizi katika Mgodi wa Tanzanite baada ya uzalishaji kusimama.

Anabainisha kuwa Mgodi wa Tanzanite una leseni ya uchimbaji Na. 490/2013 iliyotolewa Juni 20, 2013 kwa umiliki wa hisa 50:50 kati ya Shirika la Madini la Taifa na Kampuni ya TanzaniteOne Mining Ltd (TML).

Anasema uendeshaji wa mgodi huo, ulisimamishwa Desemba 2017 kufuatia kurudishwa serikalini kwa leseni ya uchimbaji ili serikali na mbia wafanye majadiliano juu ya ubia wa kampuni na mgodi.

"Kulingana na ripoti ya msimamizi wa mgodi ya Shirika la Madini la Taifa ya Septemba hadi Desemba 2019 iliyotolewa Desemba 24, 2019, uvamizi katika mgodi umeongezeka zaidi kwenye maeneo yaliyo karibu na Kitalu B ambacho kinapakana na wachimbaji wadogo.

"Ripoti imewataja wachimbaji sita waliovamia mgodi na kufanya uchimbaji. Wachimbaji hao wanadai kuwa wana vibali vya uchimbaji toka katika mamlaka husika ila hawakuweza kutoa vibali hivyo.

"Kuongezeka kwa wavamizi katika mgodi kunapunguza uhifadhi wa madini na kuharibu mazingira na miundombinu ya mgodi ambayo kwa ujumla unapunguza thamani ya mgodi na uwekezano wa mgodi kupata bei nzuri wakati wa kufanya makubaliano ya uwekezaji," CAG anatahadharisha.

Katika ripoti yake hiyo, CAG Kichere anapendekeza Menejimenti ya Shirika la Madini la Taifa, iimarishe ulinzi katika mgodi na kutatua mgongano wa uwapo wavamizi wenye vibali kwa kuwasiliana na mamlaka husika kama vile Wizara ya Madini na Tume ya Madini, juu ya madai ya utoaji wa vibali kwa wachimbaji wadogo katika mgodi huo.

**USIMAMIZI HAFIFU MASALIA**

CAG pia anasema masalia ya udongo wa uchimbaji wa madini huwa na bakaa ya dhahabu kwa kiwango kidogo, lakini ukaguzi wake juu ya usimamizi wa masalia ya udongo katika migodi ya Buhemba na Stamigold Biharamulo inayomilikiwa na Shirika la Madini la Taifa, umebaini kuwapo kwa upungufu.

Anasema Mgodi wa Buhemba una udongo wa tani 995,500 wenye kiwango cha 1.6g/t na makadirio ya uhifadhi wa dhahabu wa wakia 56,885, wakati mgodi ulipohamishwa toka kwa Kampuni ya Meremeta Mining Limited mwaka 2011.

Hata hivyo, anasema utafiti wa karibuni unaonyesha kuwa udongo huo umepungua kwa asilimia 20 hadi kufikia tani 796,400 wenye kiwango cha 1.07g/t na makadirio ya uhifadhi wa dhahabu wa wakia 30,433 kutokana na mabadiliko ya mazingira na uhifadhi usio bora wa udongo huo.

"Pia, mapitio ya ripoti ya maabara ya SEAMIC ya Septemba 2017, yanaonyesha kuwa, Mgodi wa Stamigold Biharamulo una hifadhi ya udongo wa bakaa ya uchimbaji wa madini wa tani milioni 8.35 wenye kiwango cha 0.56g/t na makadirio ya hifadhi ya dhahabu wakia 151,580.

"Udongo huu umehifadhiwa na haujachakatwa. Kutokana na ripoti hiyohiyo, kwa mwezi Septemba 2017, inakadiriwa kuwa, uhifadhi wa dhahabu utakuwa na thamani ya Dola za Marekani milioni 1113.50, sawa na Sh. bilioni 258.78.

"Kutokana na uhaba wa mtaji unaolikabili Shirika la Madini la Taifa, kama udongo huo ungechakatwa, ungeweza kuleta mapato ambayo yangesaidia ukuaji wa migodi na shirika kwa ujumla.

"Pia, uhifadhi duni wa udongo huo unasababisha upungufu na upotevu wa udongo ambao ni rasilimali muhimu. Ninapendekeza Menejimenti ya Shirika la Madini la Taifa ifanye utafiti wa uchakataji wa mabaki ya udongo wa madini na kuomba idhini ya uchakataji kama itabainika kufanya hivyo kutakuwa na manufaa makubwa kwa nchi. Pia, Menejimenti itumie njia sahihi na za kisasa za kuhifadhi masalia ya udongo wa uchimbaji wa madini," anashauri.

CAG pia anasema amebaini kuwapo kwa dosari katika utekelezaji wa sheria na Kanuni za Madini za Mwaka 2010 kuhusu usalama, afya kazini, na ulizi wa mazingira zinazomtaka mmiliki wa leseni maalum ya madini na uchimbaji kutenga fedha kama dhamana ya ukarabati ambayo inaweza kuwa kati ya Akaunti ya Escrow, Dhamana ya Mtaji, Dhamana ya Bima, au dhamana ya benki.

Anasema alibaini Migodi ya Tanzanite One Limited na Stamigold Biharamulo haikuwa imetenga dhamana hizo za ukarabati wa migodi kama ilivyoelekezwa.

Pia, Shirika la Madini la Taifa halikusimamia vizuri kiasi kilichohamishiwa kwake wakati wa kuuchukua Mgodi wa Stamigold Biharamulo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Umakini, busara muhimu kuelekea dirisha la usajili

**DIRISHA** la usajili kwa ajili ya wachezaji watakaoshiriki katika msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi Daraja la Kwanza, Ligi Daraja la Pili na mashindano ya Kombe la FA, bado halijafunguliwa rasmi.

Hii ni kutokana na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kusubiri kumalizika kwa msimu huu wa 2019/20 ambao umesimama kutokana na kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa Corona (COVID 19).

Hata hivyo, baadhi ya klabu zimeanza mchakato huo kwa kuwaongezea mikataba wachezaji wao ambao mikataba yao ya awali ilikuwa inaelekea ukingoni, lakini zipo timu nyingine bado hazijaacha mchakato huo ambao hutoa sura halisi ya kikosi.

Ili kupata kikosi imara, Nipashe inazishauri timu kuwa makini katika kufanya uamuzi wa kusajili kwa kuweka malengo.

Timu inapokuwa na malengo ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika au michuano ya Kombe la Shirikisho, lazima itasajili wachezaji wanaofanana na mashindano hayo.

Huwezi kusema unataka kufanya vizuri kwa kusajili wachezaji ambao hata kukabiliana na ushindani uliopo kwenye Ligi Kuu Bara hawana, viongozi wa timu huu ndio wakati wa kujipanga ili kuhakikisha klabu zenu zinasajili vikosi bora.

Nipashe tunazikumbusha timu zote kusajili kwa kuzingatia mahitaji halisi ya timu na kama watafanya tofauti na mapendekezo ya benchi la ufundi, watakuja kujuta pale mambo yatakavyokwenda tofauti msimu mpya utakapoanza.

Suala la usajili lisiwe la kushindana au kusajili kwa kukomoana, usajili usifanyike kisiasa au kukomoana, hii itasababisha timu kuwa wasindikizaji kwenye ligi na mashindano mengine watakayoshiriki.

Kusajili ovyo kwa kufuata mkumbo kutaleta maumivu makubwa hapo baadae kwenye timu, wachezaji wanaosajiliwa wanahitaji kulipwa mshahara kila mwezi.

Kusajili wachezaji wengi ambao kutawafanya wengine kukaa nje kunaweza kukaiongezea klabu gharama za kujiendesha jambo ambalo linaweza kuepukika kwa kusajili kwa kufuata misingi na mahitaji halisi.

Haitapendeza kusajili wachezaji wengi ambao wengine hawatakuwa na uhakika wa namba na kujikuta klabu zinawalipa mshahara wa bure.

Wachezaji pia wanatakiwa kufanya maamuzi sahihi kwa kusaini kwenye timu ambazo wanaamini watakwenda kuendeleza vipaji vyao na kuacha kuangalia maslahi peke yake.

Kukaa benchi au kukosa namba ya kudumu si jambo zuri kwa mchezaji na vile vile klabu zinatakiwa kuwa wepesi kuruhusu nyota ambao wanahitajika mahali kwingine baada ya hapo walipo kusotea benchi.

Mara nyingine tumeshuhudia timu za Ligi Kuu zikisajili kwa mbwembwe bila kufuata mahitaji husika, hali ambayo baadaye hujilaumu kwa uamuzi huo wa ovyo walioufanya.

Wakumbuke wachezaji watakaosajili wanahitaji mishahara, sasa ni lazima viongozi wahakikishe wanasajili wachezaji ambao watatumika na kulipwa mishahara kwa haki.

Timu yenye malengo, kamwe haiwezi kusajili mchezaji eti tu kuikomoa klabu nyingine, haiwezi kusajili kwa kukurupuka au kufuata mkumbo ambao baadaye husababisha hasara.

Nipashe inaamini kila upande utakuwa makini katika kutekeleza mchakato huu kwa faida ya kuendeleza vipaji vya wanasoka wa hapa nchini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

Na Barnabas Maro

# Yanga hatuna fadhila!

**"FADHILA"** ni jambo jema ambalo mtu humfanyia mwingine; hisani au wema anaofanyiwa mtu. Maneno ya shukrani kwa wema mtu aliotendewa.

"Huruma" ni hisia ya wema kwa mtu mwingine; moyo wa imani, wema na upole. 'Huruma' ni onesha moyo wa imani, onea imani.

Pamoja na hayo yote, Mungu anatukumbusha na kutuasa: "Nijaposema kwa lugha za wanadamu na za malaika, kama sina upendo, nimekuwa shaba iliayo na upatu uvumao." (1Wakorinto 13:1).

"Upendo huvumilia, hufadhili; upendo hauhusudu; upendo hautakabari, haujivuni; haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya; haufurahii udhalimu, bali hufurahi pamoja na kweli; huvumilia yote, huamini yote; hutumaini yote, hustahimili yote." (1Wakorinto 13:4-8).

Kuna mtu anayeitwa Jella Mtagwa. Huyu alikuwa mcheza kandanda maarufu si kwa klabu za Yanga na Pan African tu, bali pia kwa Timu ya Taifa (Taifa Stars).

Umuhimu na umaarufu wa Mtagwa ulipewa uzito na Shirika la Posta Tanzania (wakati ule) kwa kuweka picha yake kwenye stempu.

Hakuna mchezaji mwingine wa Tanzania aliyepewa heshima hiyo ila ni Mtagwa. Tuzo ni kitu anachopewa mtu kama zawadi baada ya kufanya jambo jema au kazi nzuri; tunu.

Zamani nilifuga paka aliyenizoea sana. Kila niliporudi nyumbani nilihakikisha namletea mishikaki. Alinisubiri mlango wa mbele ili kuniona nirudipo.

Aliponiona alinikimbilia na 'kunipokea' kwa wimbo wa 'nyau, nyau, nyauu ...' na kuingia naye ukumbini. Nilipompa mishikaki alijituliza na kula, kisha kunifuata na kujipitishapitisha miguuni mwangu kuonyesha shukrani.

Kama wanyama wanajua kushukuru, iweje binadamu tunashindwa kuwashukuru wenzetu wanaotufanyia mambo mazuri? Upendo wetu uko wapi?

"Zaidi ya hayo yote jivikeni upendo, ndio kifungo cha ukamilifu. Na amani ya Kristo iamue mioyoni mwenu, ndiyo mliyoitiwa katika mwili mmoja; tena iweni watu wa shukrani." (Wakolosai 3:14-15).

Hapa kuna watu wa makundi matatu wanaostahili lawama kwa kutomsaidia Mtagwa ambaye sasa anaugua kiharusi.

Kwanza ni viongozi wa vilabu vya Yanga na Pan African wakiwamo wanachama na mashabiki wao. Pili ni Shirikisho na Soka Tanzania (TFF) na mwisho ni Chama cha Wachezaji wa zamani wa vilabu, hasa Simba, Yanga na Taifa Stars.

Kwa nini timu hizo zashindwa kuwahudumia wachezaji wao wa zamani wanapopatwa na maradhi au kutojimudu hata kuishi maisha ya shida?

Tumeona au kusikia wachezaji kadhaa wa timu mbalimbali waliougua na hatimaye kupoteza maisha bila kupata msaada wowote wa vilabu walivyovitumikia kwa mafanikio makubwa. Aibu iliyoje!

Chama cha wachezaji wa zamani kiko wapi? Au kimelala usingizi wa pono (samaki wa wastani wa rangi ya kijani mwenye meno mapana na mnofu laini anayeishi sehemu zenye mwani na anayependa kutulia kama aliyelala)?

Waandishi wa zamani na waliopo hawajui umuhimu wa chama chao? Wakumbwapo na matatizo humlilia nani? Hawaoni jinsi wenzao wanavyobabaishwa kulipwa stahiki zao?

Kabla ya kusaini kwenye vilabu vinavyowasajili, mwanasheria wa chama cha wachezaji anapaswa kuona mikataba yao kabla na kujadiliana nao kama wanaridhika ama la.Wanapokubaliana ndipo wachezaji watie saini.

Walipwe fedha kamili za usajili na marupurupu mengine kama yapo. Pia walipwe mishahara yao kila mwisho wa mwezi bila kubabaishwa.

Turudi kwenye suala la Mtagwa. Yanga na Pan African zichangishe hela za klabu na wanachama au mashabiki ili kumsaidia nyota huyo na pia wakamwombe radhi kwa kutomsaidia.

Vilabu hivyo vyapaswa kuitisha mikutano ya dharura na kuyashauri matawi yao kote nchini yakae na wanachama/wapenzi kumchangia Mtagwa.

Kadhalika TFF nayo ifanye mpango wa kupata fedha za kwenda kumsaidia Jella. Pia wamwombe msamaha kwa kutomsaidia, ingawa aliiletea Tanzania sifa na picha yake kuwekwa kwenye stempu za Posta.

"Tamu tulikula sote na uchungu vumilia." Maana yake tulishirikiana wakati ar aha sasa yapasa kuuvumilia uchungu au kuyakabili matatizo.

Je, chama cha wachezaji wa zamani kina mkakati gani kama uliofanywa na kundi la WhatsApp la Sports Vision likiongozwa na Bakari Malima na Mkala Fundikira waliokwenda kumkabidhi Mtagwa Sh. 500, 000/-?

Walichofanya jamaa hao ni msutano (tendo la kukosoana na kuambiana kweli ana kwa ana) na fedheha kwa waliopaswa kumjulia hali mchezaji wao wa zamani!

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

HABARI KITAIFA

# Bei ya barakoa changamoto

**Na Waandishi Wetu**

Upatikanaji wa barakoa kwa ajili ya kujikinga na maambukizi ya corona umelalamikiwa katika maeneo kadhaa nchini kutokana na bei kuwa kuwan.

Jijiji Dar es Salaa katika baadhi ya maeneo,

bidhaa hiyo inazuwa kati ya Sh. 1,000 hadi 3,000, huku kitaalamu ikitakiwa kuvaliwa kwa saa nne na kubadilishwa.

Aidha, maji tiba yanauzwa kati ya Sh. 5,000 hadi 10,000 kutegemeana na ujazo, kiasi ambacho ni kikubwa kwa mwananchi wa kawaida kumudu gharama.

Baadhi ya wananchi waliiomba serikali kuangalia uwezekano wa kusambaza vifaa hivyo ili vipatikane kwa bei rahisi au kugawiwa bure.

Shabani Asumani, mkazi wa Tabata, alisema kuna baadhi ya sehemu wafanyabiashara wanatumia kigezo cha uhitaji mwingi wa bidhaa hizo kufanya ulanguzi.

Alisema baadhi yao wamepandisha bei mara mbili ya kiasi halali cha uuzwaji wa bidhaa hizo pamoja na watu wengi kuzihitaji kwa wingi kipindi hichi cha sikukuu ili zitumike kwa wageni wanaotembelea ndugu.

Jema Iddy (34), mkazi wa Bima ambae pia ni mfanyabiashara wa vifaa hivyo, alisema wanauza kwa bei ambazo zinawasaidia kurudisha fedha walizo tumia kununua vifaa hivyo.

Alisema baadhi ya wananchi wanalalamikia wafanyabiashara kuwa wanapandisha bei ya vifaa hivyo pasipo kujua kuwa wao wanavipata kwa gharama gani wanapoenda kufungasha katika maduka makubwa.

**KIbaha changamoto**

Baadhi ya wakazi wa Kibaha mkoani Pwni, wamesema bado kuna changamoto katika upatikanaji wa vifaa vya kujikinga na virusi vya corona hususani barakoa.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti walisema, awali vitakasa mikono vilikuwa vinapatikana kwa shida, lakini kwasasa changamoto imetafutiwa ufumbuzi kilichobaki ni upatikanaji wa barakoa.

Shabani Matimbwa, mmoja wa wakazi wa Kwamatias alisema, barakoa ambazo awali zilikuwa zikipatikana katika maduka ya vifaa vya ujenzi sasa hazipatikani kwa urahisi.

Matimbwa alisema, zenye ubora zinauzwa kati ya Sh. 4,000 hadi 5,000 na zenye ubora hafifu zinauzwa Sh. 2,000 ambazo upatikanaji wake ni wa shida.

"Kujikinga na huu ugonjwa wa corona inahitaji tutumie vifaa vinavyoelekezwa na wataalamu wa afya, lakini vifaa hivi kwa wananchi wa hali ya chini bado ni changamoto, upatikanaji wake wa shida na gharama ya ununuzi iko juu, tunaomba serikali iangalie namna ya kutusaidia," alisema.

Naye Diwani wa Kata ya Mailimoja, Ramadhani Lutambi alisema, barakoa hizo matumizi yake kwa mujibu wa watalaamu wa afya yanahitaji umakini kwa kuzibadilisha mara kwa mara kwa kwa hali za wananchi wa kipato cha chini kwao itakuwa changamoto.

Baadhi ya maduka ya dawa za binadamu, maduka ya vifaa vya ujenzi na ya vifaa vya shule ambayo yalikuwa yanauza barakoa kwa sasa hazipatikani kwa wingi na bei zimepanda kutoka Sh. 2,000 na hadi 5,000 kwa moja.

**Iringa malalamiko**

Katika maduka ya mjini Iringa, imeleta utata baada ya kila duka kuuza kwa bei yake hatua iliyowafanya wananchi kuiomba serikali kutangaza bei elekezi.

Uchunguzi uliofanywa na mwandishi wa habari hizi katika baadhi ya maduka, umebaini kuwa bei ya barakoa katika maduka ya mji wa Iringa inatofautiana.

Maduka ambayo yamehusika katika uchunguzi ni yanayouza dawa na vifaa tiba. Uchunguzi ulibaini katika baadhi ya maduka, barakoa za aina mbili tofauti zilikuwa zikiuzwa kwa Sh. 15,000 na 3,000.

Pia uchunguzi umebaini katika baadhi ya maduka barakoa hizo zilikuwa zinauzwa kwa Sh. 3,000 na 1,500 huku katika duka moja la dawa wakiuza kwa Sh. 1000.

Wakizungumza kwa sharti la kutoandikwa majina yao gazetini, wasemaji wa baadhi ya maduka hayo ya dawa walisema, barakoa zinauzwa kila mmoja na bei yake kutokana na gharama waliyonunulia pamoja na ubora wake.

Hata hivyo, walisema hivi sasa maduka mengi yana upungufu wa vifaa hivyo kutokana na wanakozichukua kuwa na uhaba mkubwa jambo linalosababisha bei wanazouzia kuwa tofauti.

Amina Ally, mkazi wa Miyomboni, alisema kwa kuwa vifaa hivyo ni muhimu kwa ajili ya kujikinga, ni vyema serikali ikaangalia uwezekano wa kuweka ruzuku yake ili wafanyabiashara hao waweze kuuza kwa bei elekezi.

Alisema kutokana na hali ya ugumu wa maisha, kwa sasa mtu kuuziwa barakoa kwa Sh. 15,000, kifaa ambacho kinatumika kwa muda ni gharama kubwa.

Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Richard Kasesela, alisema vifaa hivyo kila mmoja anauza kwa bei yake kutokana na kutowekwa bei elekezi na serikali.

**Imeandikwa na Maulid Mmbaga, Dar,**



Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, akinawa mikono kujihami na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona, kabla ya kuingia katika mkutano na maofisa wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Tanga (TANGAUWASA), alipofanya ziara mkoani Tanga mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Ofisa Uhusiano wa mamlaka hiyo, Anna Makange. **PICHA: DEGE MASOLI**

# Mkuu mstaafu wa KKKT afariki dunia

**Na Romana Mallya**

ALIYEKUWA Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Samson Mushemba (85), amefariki dunia katika Hospitali ya Ndolage, Kamachumu wilayani Muleba, mkoani Kagera.

Dk. Mushemba ambaye ni Askofu mstaafu wa KKKT Dayosisi ya Kaskazini Magharibi (Bukoba), alifariki juzi usiku wakati akiendelea na matibabu hospitalini hapo.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkuu wa Kanisa la KKKT, Dk. Fredrick Shoo, alithibitisha kutokea kwa kifo hicho na kueleza kanisa linaendelea kuwasiliana na familia na wamekubaliana ibada ya mazishi itafanyika Jumatano ya wiki ijayo. Dk. Mushemba alikuwa Mkuu wa KKKT tangu 1992 -2007 baada ya kifo cha Askofu Dk. Sebastian Kolowa (1976 - 1992) ambaye alipokea wajibu huo kutoka kwa Askofu Dk. Stephano Moshi (1963-1976).

# Kero wizi fedha za bidhaa mtandaoni kushughulikiwa

**Na Mwandishi Wetu**

KERO ya wizi wa fedha za bidhaa mtandaoni iliyokuwa ikiwakabili Watanzania wengi, imepata ufumbuzi.

Ufumbuzi huo umetokana na kampuni tanzu ya Libazon Holdings ya Uingereza kuanza kutoa huduma hiyo nchini.

Meneja uendeshaji wa kampuni hiyo, Daniel Gaudence, akizungumza na Nipashe, alisema kwa muda mrefu Watanzania wamelalamikia kuibiwa kwa biashara za mtandaoni, hivyo wamefungua ofisi kuhakikisha kuwa huduma zinawafikia wananchi kirahisi.

Alisema Libazon Tanzania itakuwa na jukumu la kupokea mizigo kutoka nje ya nchi na kuwafikishia wateja kokote waliko kulingana na walivyoagiza.

"Wateja wetu wamerahisishiwa, wanaweza kulipia bidhaa kwa simu, benki, kadi au fedha taslimu. Tunaruhusu wateja kuuliza jambo lolote, lengo ni kuwaridhisha na bidhaa wanazozipata ikiwa ni kutoka nje ya ndani ya nchi," alisema.

Gaudence alisema jukwaa hilo ni kama soko linaloruhusu biashara au wauzaji binafsi kutumia fursa ya kuwafikia wateja wengi nchini bila kuwa na duka halisi, na kwamba wanatoa huduma nyingine kama ukusanyaji wa malipo, habari ya uuzaji, ufugaji na usafirishaji ikiwamo kupanga mapato kwa pamoja kama yapo.

Kwa mujibu wa Gaudence, moja ya changamoto ya biashara mtandaoni ni uaminifu wa kuhakikisha bidhaa zinawafikia wahusika jinsi walivyozichagua na kwamba watu wengi wamepoteza fedha zao kwa muundo huo, na kwamba kampuni hiyo imekuja tofauti na inawahakikishia huduma bora.

Meneja huyo alisema nyingine ni soko kujaa bidhaa bandia na hivyo kupoteza imani kwa watu, huku ikiongeza uwanja usio sawa wa kushindana kibiashara baina ya wanaouza bidhaa bandia na halisia.

"Tume ya Ushindani Bora (FCC), inashughulikia changamoto hii, lakini bado nguvu zaidi inahitajika, Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (TCRA) na kwa kweli jeshi la polisi la Tanzania limesifiwa kwa kuchukua hatua madhubuti kukomesha utapeli unaotokana na uhamishaji pesa ambao ni sehemu muhimu katika mafanikio ya bishara mtandaoni,' alisema.

# Wawili wapya wa corona wagundulika

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAGONJWA wawili wapya wa corona wamegundulika Zanzibar na kufanya idadi ya wagonjwa kufikia tisa ambao wamewekwa chini ya uangalizi katika kambi maalumu ya Kidimni, Wilaya ya Kati Unguja.

Waziri wa Afya, Hamad Rashid Muhammed, amethibitisha kuwapo kwa wagonjwa hao ambao ni wanaume na raia wa Tanzania.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari, alisema wagonjwa hao mmoja ana umri wa miaka 33 ambaye ni mkazi wa Muembe Tanga, mjini Zanzibar na mwingine miaka 24 mkazi wa Mwanakwerekwe.

Alisema wagonjwa hao hawana historia ya kusafiri nje ya nchi kwa hivi karibuni.

Pia, alisema Wizara ya Afya inaendelea kuwafuatulia watu wa karibu waliowahi kukutana na wagonjwa hao ili kudhibiti kuenea kwa maambukizi mapya.

"Hadi kufikia April 9 saa 8:00 mchana, jumla ya watu 86 waliokutana na wagonjwa hao wanafuatiliwa pia kuna watu 252 waliorudi kutoka nje ya Tanzania wamewekwa karantini," alisema.

Alisema kuwa watu 202 wameruhusiwa kutoka karantini baada ya kukaa kwa siku 14 na kutoonyesha dalili zozote za maradhi hayo.

Hamad aliwataka wananchi kuchukua tahadhari zote na kuzingatia maelekezo ya serikali na wataalamu wa afya ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa wa corona.

Alisema kinga ni bora kuliko tiba hivyo ni vyema kuchukua tahadhari kuliko kusubiri mpaka maradhi yaathiri kwa kiwango kikubwa.

# Kanisa latoa tamko uchaguzi mkuu

**Na Romana Mallya**

KANISA la Katoliki Tanzania limewataka Watanzania kuutumia uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika mwezi Oktoba, mwaka huu, kuchagua viongozi wanaowataka na kuwakataa wanaojileta wenyewe kwa tamaa za madaraka na rushwa.

Kupitia ujumbe wao wa Pasaka kwa kanisa, uliosomwa jana na Askofu wa Jimbo la Mbulu mkoani Manyara, Anthony Lagwen, ulisema kuwa viongozi watakaochaguliwa wawe wanaomcha Mungu.

"Viongozi tutakaowachagua wawe ni wale wanaomcha Mungu, siyo wanaotegemea udanganyifu wa nguvu zao, wenye fikra za upuuzi kama ushirikina.

"Ukweli ni kwamba, viongozi wanaochaguliwa kwa uhuru, haki na usawa kwa kadiri ya matazamio ya wote ni wa mpango wa Mungu. Sauti ya wengi ni sauti ya Mungu.

"Warumi 13:1, wenye mamlaka wamewekwa na Mungu, wanaojali na kutanguliza maslahi mapana ya nchi yetu siyo wenye tabia ya ubinafsi na ubaguzi wa aina yoyote."

Pia, ujumbe huo wa pasaka uliwaeleza waumini kwamba, wanahitaji viongozi waungwana, waliopambwa kwa fadhila njema za kimungu na wenye kuheshimu tunu muhimu za kijamii za kujali ukweli, uhuru na usawa kati ya raia wote.

Uliwataka waumini kuwajibika kwa upendo, kulinda, kutunza na kuiombea amani ya nchi.

"Tunawasihi Watanzania kushiriki ipasavyo kwa kadiri ya nafasi zenu kutayarisha mazingira mazuri ya kufanyika uchaguzi kwa kuzingatia misingi iliyo huru na ya haki ambayo matunda yake yatakuwa amani."

Kadhalika, iliwataka watumie haki yao ya kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kadiri ya vigezo vilivyopo kwa mujibu wa sheria za uchaguzi.

"Kila anayehusika kwa mfano, anayeratibu, anayetaka kuchaguliwa, anayepiga kura, anayesimamia, anayehesabu kura awe mwaminifu, aongozwe na dhamira safi.




Mwendesha bodaboda akivunja sheria za usalama barabarani kwa kupakia abiria wawili maarufu kama 'mshikaki' huku wote wakiwa hawajavaa kofia ngumu ya kukinga kichwa 'helmet' katika Barabara ya Kawawa, eneo la Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Msekwa aona uwezekano uchaguzi urais kupingwa

**Na Enock Charles**

SPIKA mstaafu, Pius Msekwa, amegusia uwezekano wa matokeo ya urais kupingwa mahakamani kutokana na mazingira na siasa za miaka ya hivi karibuni kuwa tofauti na hali ilivyokuwa zamani.

Akihojiwa na chombo kimoja cha habari jijini Dar es Salaam, alisema kwa mazingira ya wakati ule (akiwa kwenye siasa) enzi za uongozi wa Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, uchaguzi ulikuwa unasimamiwa vizuri na malalamiko katika kura za Urais hayakuwapo kwa kiwango kikubwa tofauti na hali ilivyo sasa.

"Kwa mazingira ya wakati ule wa Mwalimu Nyerere, uchaguzi ulikuwa unaendeshwa vizuri kabisa, hakuna malalamiko yaliyokuwa yanatokea hasa kuhusu uchaguzi wa Rais," alisema Msekwa.

"Malalamiko yalikuwa yanatokea kwenye baadhi ya chaguzi za wabunge na yalikuwa yanafika mahakamani, lakini kwa sasa nakubali kuwa mazingira yamebadilika na Katiba iliyopendekezwa na Warioba imeweka kifungu hicho kwa hiyo sasa hakuna tena ubishi," alisema.

Kuhusu udhibiti wa rushwa, alisema vita dhidi ya rushwa ni jambo endelevu na kwamba jambo la msingi ni kwa uongozi uliopo madarakani kupambana kwa kadri inavyowezekana kuipunguza ili isiathiri maendeleo na ukuaji wa uchumi.

"Tatizo la rushwa linajulikana dhahiri kabisa, kwa wakristo, wanajua rushwa ilianza wakati wa Yesu wale askari waliokuwa wanamlinda walipewa rushwa ili wasiseme kuwa kafufuka imeumbwa pamoja na binadamu," alisema.

"Kama nchi, kama Serikali, mnaweza kupigana nayo kwa kutumia Sheria hakuna njia nyingine na sheria za rushwa tunazo katika nchi yetu, tunavyo vyombo vya kupambana na rushwa na mahakama pia ipo," alisema Msekwa.





# Mavunde atoa saruji kutatua uhaba madarasa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma, inakabiliwa na uhaba wa vyumba vya madarasa 1,900 kwa shule za msingi na sekondari.

Mbunge wa Jimbo la Dodoma mjini, Anthony Mavunde, ametoa matofali 40,000 na mifuko ya saruji 1,320 kwa kata zote ili kutatua kero ya miundombinu kwenye shule hizo.

Akikabidhi matofali na saruji jana, Mavunde ambaye pia ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, alisema vitu hivyo vimetolewa kupitia fedha za mfuko wa jimbo.

Alisema lengo kubwa ni kusaidia ujenzi wa vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo na nyumba za walimu na kuwataka viongozi wa kata kuhakikisha wanasimamia vyema matumizi ya vifaa hivyo.

"Ndani ya kipindi cha miaka minne hadi sasa nimetoa matofali 100,000 na mifuko 11,000 ili kutatua kero zinazoikabili sekta ya elimu, na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia,"alisema.

Vile vile, alisema sekta ya elimu ni pana na kila mmoja ana wajibu wa kuungana na serikali ili kuhakikisha wanafunzi wanasoma katika mazingira mazuri.

"Mimi nitaendelea kuunga mkono jitihada za Jiji la Dodoma ambalo ni miongoni mwa halmashauri chache nchini zilizotenga fedha nyingi kutatua changamoto zilizopo kwenye sekta ya elimu," alisema.

Naye, Ofisa Takwimu wa halmashauri hiyo, Debora Muwinje, alisema saruji na matofali hayo yametolewa kwa shule za msingi 38 na mbili za sekondari.

Ofisa Elimu Msingi wa halmashauri hiyo, Joseph Mabeyo, alisema halmashauri hiyo imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali kukabiliana na upungufu wa vyumba vya madarasa 1,900.

Alisema mwaka wa fedha 2020/21 kimetengwa kiasi cha Sh. bilioni saba kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya shule hizo.

# Watupa taka vifungashio ovyo kukiona

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imetangaza kuwachukulia hatua za kisheria wafanyabiashara wanaosababisha kusambaa ovyo taka za vifungashio vya matunda sokoni.

Hatua hiyo ilitolewa jana na Ofisa Masoko wa jiji hilo, James Yuna, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu suala la utupaji wa taka zinazotokana na bidhaa za matunda zinazoletwa na wafanyabiashara wa nje ya jiji.

Alisema kwa sasa jiji hilo litaanza kutoza faini kwa magari yote na wale watakaobainika kutupa vifungashio hivyo kwenye madampo yasiyo rasmi ya kutupa taka hizo. Yuna alisema kuwa vifungashio hivyo havipaswi kuachwa na kutupwa kwenye madampo yaliyopo kwenye masoko bali taka hizo zinatakiwa kupelekwa dampo lililotengwa Chidaya Ntyuka.

Alisema hivi sasa kuna baadhi ya wafanyabiashara wanaoleta bidhaa za matunda zikiwa zimefungashwa na majani na wakishusha huyaacha sokoni. Alibainisha kuwa wanaofanya kitendo hicho wanakiuka kanuni na sheria.

"Halmashauri imeshatoa katazo juu ya vifungashio hivyo vinavyoletwa kwenye masoko yake na tumewataka wafanyabiashara wote wanaoleta na kushusha bidhaa zao zikiwa kwenye vifungashio baada ya kumaliza kuondoka navyo na kupeleka dampo la Chidaya kulikopangwa kutupa takataka zote," alisema.

Hata hivyo, alisema baadhi ya masoko ya jiji hilo imebainika kuwa madampo yake wafanyabiashara wanakiuka kanuni za usafi kwa kutupa vifungashio hivyo vilivyopigwa marufuku na halmashauri. Ofisa huyo alitaja masoko hayo yanayotupa taka za vifungashio hivyo kuwa ni pamoja soko la matunda na samaki wabichi la Bonanza na soko kuu la Majengo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Idara ya mazingira na taka ngumu wa Jiji hilo, Dickson Kimaro, alisema Halmashauri itahakikisha inachukua hatua kali kwa wale wanaokiuka utaratibu na sheria.



Mkulima wa uwele, Cesilia Machite, akikagua mazao yake shambani kwake, Hombolo nje kidogo ya Jiji la Dodoma juzi. Zao hilo, limekuwa ni mkombozi kwa wakulima kutokana na kuvumilia ukame. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waislamu waonywa kuhamasisha migogoro

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SHEKHE wa Mkoa wa Dodoma, Alhajji Mustafa Shabani, amewataka viongozi wa Baraza Kuu la Waislamu (Bakwata), ngazi zote kuacha kuhamasisha migogoro ndani ya baraza hilo kwa kuwa inawarudisha nyuma kimaendeleo.

Pia, amesema kiongozi atakayebainika kuchochea migogoro ndani ya misikiti atachukuliwa hatua za kinidhamu.

Kauli hiyo aliitoa jana alipokuwa akizungumza na viongozi hao kwenye kikao cha mkutano mkuu wa uchaguzi wa Baraza hilo, Wilaya ya Dodoma.

Alisema kuwa imezuka tabia kwa baadhi ya viongozi ndani ya Bakwata kuwa chanzo cha kuchochea na kuhamasisha migogoro.

Shekhe huyo alisema hategemei katika uongozi wake kuwa na viongozi wa aina hiyo wanaowagawa Waislamu badala ya kuwaweka pamoja.


"Napenda niseme wazi kwenu nyinyi viongozi wa ngazi ya wilaya mtakaochaguliwa hapa, sitarajii kufanya kazi ndani ya Bakwata na viongozi wasiopenda maendeleo ambao badala yake wanahamasisha migogoro inayorudisha nyuma uislamu wetu," alisema.

Akifungua mkutano huo, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde, aliwataka viongozi na waumini wa dini ya Kiislamu kuhakikisha wanaheshimu katiba yao na kuwa waadilifu kwenye uongozi wao.

Mavunde alisema Baraza hilo linatakiwa kuwa na viongozi makini na wasikivu na wasiokuwa na dosari yoyote ya kusababisha vurugu na kuuchafua uislamu.

Aliwahimiza kujenga umoja, upendo na mshikamano katika kukuza uislamu na kuchochea maendeleo.

Naye, Mwenyekiti Mpya wa Baraza la Halmashauri ya Bakwata Wilaya ya Dodoma Ustadhi, Bashiru Hussein, alisema atahakikisha anawaunganisha waislamu bila kubagua.





Waziri wa Afya Zanzibar, Hamad Rashid Muhammed, akitoa taarifa kwa waandishi wa habari jana, kuhusu kuongezeka kwa wagonjwa wapya wawili wa corona na Zanzibar kuwa na idadi ya wagonjwa tisa. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Watoto wenye mahitaji maalumu kupata elimu bora

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali, imesema inaendelea kuzitafutia ufumbuzi changamoto zote zinazowakabili watoto wenye mahitaji maalumu ili kuhakikisha wanapata elimu bora itakayowasaidia kuendeleza maisha yao.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa maoni na maagizo ya kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi ya mwaka 2019/2020, Kaimu Waziri wa wizara hiyo, Mahmoud Thabit Kombo, alisema miongoni mwa hatua za kupunguza changamoto hizo ni kukamilisha sera ya elimu mjumuisho ambayo imezingatia kuimarisha mazingira mazuri ya kuwapatia elimu watoto wote wenye mahitaji maalumu.

Alisema pamoja na jitihada za wizara, bado kunachangamoto ya upatikanaji wa elimu bora kwa baadhi ya watoto wenye ulemavu hasa wenye matatizo ya akili. Pia, alisema katika hatua nyingine za kuboresha elimu hapa nchini, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inahakikisha kuwa shule zote zinapatiwa mahitaji muhimu ya kufundishia na kujifunza ikiwamo chaki, madaftari, vitabu na vifaa vya maabara.

Alisema hatua nyingine iliyochukuliwa ni serikali kufuta rasmi michango yote katika shule za sekondari na badala yake kila mwanafunzi katika shule hizo atapatiwa Sh. 33,000 zitakazoingizwa katika akauti ya shule kusaidia uendeshaji.

Akitoa maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mwanaasha Khamis Juma, alisema ni vyema Wizara ya Elimu ikaimarisha kitengo chake cha elimu mjumuisho kwa kukipatia usafiri pamoja na kukipa nguvu zaidi kwa kuajiri walimu wenye fani hiyo.

Kwa upande wao baadhi ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamezipongeza shule binafsi kwa mchango mkubwa wanaotoa wa kusaidia upatikanaji wa elimu.

Hata hivyo, walisema licha ya mchango mkubwa wa shule hizo, bado kuna baadhi ya shule za binafsi zinawakataa wanafunzi ambao wameshuka kimasomo.

# Wakristo watakiwa kuchukua tahadhari Pasaka

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mkoa wa Mjini Magharibi, imewataka waumini wa dini ya Kikristo kufanya ibada na kusherehekea Sikukuu ya Pasaka kwa kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya ili kujikinga na maambukizi ya maradhi ya corona.

Hayo yalielezwa na Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi Hassan Khatib Hassan, wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Vuga, mjini Zanzibar. Alisema waumini hao wana wajibu wa kufanya ibada na kusherehekea sikukuu, hivyo ni vyema tahadhari za makusudi zikachukuliwa kuepusha mkusanyiko kulingana na hali ya maradhi ilivyo.

"Sisi kama viongozi wa serikali tunajua umuhimu wa ibada na sikukuu hii na serikali ipo pamoja nao, lakini mazingira si salama sana kwa hivyo tunawaomba wenzetu wafanye ibada kulingana na maelekezo ya wataalamu wa afya," alisema.

Aliwataka waumini hao wanapomaliza ibada warudi nyumbani kuepusha mikusanyiko kwa kuwa usalama wa afya ni jambo muhimu.

Hassan aliwataka viongozi wa madhehebu mbalimbali ya dini ya Kikristo kusimamia na kutekeleza maelekezo hayo ya serikali kwa kuwaelimisha waumini wao madhara ya maradhi ya corona.

Alisema ni vyema wanapofanya ibada zao kanisani kukaa umbali wa mita moja na nusu baina ya mtu na mtu na kuachana na mialiko ili kujikinga na ugonjwa huo.

Hata hivyo, aliwataka viongozi wa dini kufupisha muda wa mahubiri na sala na mahubiri yao yaelekeze katika utoaji wa elimu juu ya maradhi hayo ikiwa na lengo la kuchukua tahadhari ya kuwakinga waumini.

Alisema serikali ya mkoa kupitia kamati ya ulinzi na usalama itaendelea kuimarisha ulinzi na usalama kwa kipindi chote cha sikukuu na kuwataka wananchi kubaki majumbani pale wanapomaliza shughuli zao za msingi.

# Magofu Zanzibar yatumika kutangaza utalii

**Na Rahma Suleiman**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema itatumia utajiri wa magofu ya kale ya kihistoria yaliopo Zanzibar kwa ajili ya kutangaza na kukuza sekta ya utalii nje ya nchi.

Waziri wa Habari Utalii na Mambo ya Kale, Mahmoud Thabit Kombo, alisema mikakati ya wizara ni kuimarisha magofu ya kale kuwa moja ya sehemu ya utalii utakao wawezesha wageni kujua historia ya Zanzibar na watawala.

Kombo alisema hayo wakati akifafanua taarifa ya kamati ya maendeleo ya wanawake na utalii ya Baraza la Wawakilishi ambayo iliwasilisha taarifa yake katika Baraza hilo.

Alisema juhudi kubwa zimechukuliwa na wizara ikiwamo kuyafanyia ukarabati mkubwa magofu ya kwa Bihole yaliopo Bungi pamoja na Mwinyimkuu yaliopo Dunga wilaya ya Kati Unguja.

Alisema magofu ya Bihole na Mwinyimkuu, ukarabati wake umetumia Sh. bilioni 1.19 na kurudisha haiba yake ya zamani.

Aliwaambia Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba tayari magofu ya kale ya Bihole yamegeuzwa kuwa kituo cha utamaduni wa mambo ya kale na kutoa fursa na nafasi kwa watalii kutembelea maeneo hayo.

"Mheshimiwa Spika, tumefanya ukarabati mkubwa wa magofu ya Bihole yaliopo Bungi ambayo kwa sasa tumeyageuza na kutangaza kuwa kituo kikuu cha utamaduni wa mambo ya kale ambacho kitatoa fursa kubwa kwa watalii na wageni na watu wanaofanya mambo ya utafiti kupata taarifa za ziada," alisema.

Alizitaja faida za kufanyika kwa ukarabati wa magofu ya kale ni kutoa fursa kwa watalii na wageni mbalimbali kutembelea Zanzibar na kupata maelezo ya historia ya mambo ya kale kwa ajili ya kufanya utafiti.

"Magofu yetu ni tegemeo kwa watafiti kujuwa historia ya mambo ya kale pamoja na kujua tawala mbalimbali za kigeni za kijadi zilizotawala nchini," alisema.

Magofu ya Bihole yamejengwa katika karne ya 19, na mjukuu wa Sultani Sayyed Said ambaye anasifika kwa kuongoza ngome ya idadi kubwa ya watumwa huku akiwa mwanamke.



**CARD B ETI 'AMEMISI' FAMILIA YAKE** Soma UK.14

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI APRILI 11, 2020



## MKWARA WA LULU DIVA

# Ole wenu mtakaojibebisha

BASI SAWA

## Kumbe Chidi Benz, Barakah wapo safi

RAPA Chidi Benz, ametoboa siri kwamba yeye na msanii mwenzake Baraka The Prince, wana uhusiano wa karibu na kusaidiana kwenye matatizo.

Akizungumza kupitia EATV, Chidi Benz, amesema alimjua Barakah The Prince baada ya kupewa namba yake kipindi ambacho ana matatizo na msanii huyo alimsaidia kiasi cha fedha.

"Barakah ni mdogo wangu, hana kiburi kama wanavyosema ila ana mitazamo, kipindi fulani nilikuwa vibaya sana nilikuwa nawacheki watu waweze kunisaidia kunitumia pesa, ila nilipata namba za Barakah hata simjui maskini" amesema.



## Corona yamuibua dogo Stardrey

MSANII chipukizi wa Bongo fleva, Stardrey, ametambulisha ngoma yake mpya inayohamasisha kupiga vita ugonjwa wa corona.

Wimbo huo ambao unajulikana kwa jina la "I Do" upo katika mfumo wa Audio na umeanza kupigwa katika vituo mbalimbali vya redio na mitandao ya kijamii.

"Nimerejea rasmi katika ulingo wa muziki na natumaini wimbo huu utahamasisha watu kukaa mbali na corona," amesema Dwight Danda.





## MKWARA WA LULU DIVA Ole wenu mtakaojibebisha

MWANAMUZIKI wa BongoFleva, Lulu Diva, ametoa tahadhari kwa wanaotamani waume za watu, akisema ole wao watakaomsogelea mwanamume wake.

Lulu Diva amesema endapo ataamua kuingia katika uhusiano atakuwa mkali na atahakikisha rafiki yake yeyote, amshike mkono au kumsalimia mwanamume wake.

Msanii huyo ambaye anahusishwa kuwa karibu na Rich Mavoko kwa kipindi kirefu, amesema kwa sasa yupo huru na anaendelea kumtafuta mwanaume sahihi kwake.

Amesema anachohofia kuwa kwenye uhusiano wa kimapenzi ni kwa sababu marafiki zake wakijua itakuwa shida, ndiyo maana huwa anapendelea kuweka siri.

"Mimi naogopa kuwa kwenye uhusiano ambao marafiki zangu watajua, na nitakapokuwa nimeanza uhusiano sitamani hata rafiki yangu amshike mkono au amsalimie mwanamume wangu, maana siku hizi watu wamekaa kuangalia uhusiano wa watu kama wamegombana au wataachana lini, hawataki heri, wanapenda matatizo tu", ameeleza Lulu Diva.

## Nedy Music usingefuta ingekuwaje?

MWANAMUZIKI, Nedy Music, amesema aliamua kutumia mbinu za kimafia kwa ajili ya kulinda kazi yake mpya.

Akizungumza na ya EATV, Nedy, amesema mwenzi mmoja kabla ya kutambulisha ngoma yake mpya, alifuta ukurasa wake wa Instagram na kutotumia ili kuweka mikakati yake sawa.

"Niliamua kufuta picha zote Instagram na kukaa bila kutumia mtandao huo kwa mwezi mmoja, nilikuwa napanga mkakati wangu sawa kwa ajili ya wimbo wangu mpya", amesema Nedy.

Kuhusu kutoelewana na mtu wake wa karibu na aliyekuwa meneja wake, Ommy Dimpoz, chini ya 'lebel' ya PKP, Nedy amesema wao wawili hawana ugomvi.

Nedy ametoa wimbo mpya hivi karibuni unaojulikana kama 'Amen' ambao mpaka sasa una watazamaji takribani







## Harmonize umeyataka mwenyewe

KWELI majuto ni mjukuu! Staa wa muziki wa Bongo Fleva, Harmonize, ameajutia uamuzi wa kumuweka mke wake kama mpambaji wa video ya wimbo wake wa niteke, sasa ameapa kutorudia tena kitendo hicho.

"Mke wangu sio video vixen, ali-shoot video na mimi kwa sababu ni mume wake, hata mimi siwezi kufanya naye kazi hiyo tena, maana nikifanya hivyo itakuwa nimemuhalalisha kwamba video vixen ni kazi yake" amesema Harmonize.

Akizungumzia suala la mke wake kutozoeana na watu, wasanii na vyombo vya habari, amesema "Nilitamani iwe hivyo, ila sio kama nimeweka kwamba hatakiwi kufanya hivyo, kwa sababu tayari ameshakuwa maarufu, watu wanamuona na kumfuatilia ila natamani ingekuwa hivyo japo najua haiwezekani".

UNASEMAAA...



## Duh! Kiba ulishtukaje kumuona Hamisa?

MFALME wa BongoFleva Alikiba, amesema alishtushwa na uwepo wa mrembo Hamisa Mobetto visiwani Zanzibar, kwa sababu hakujua nani atafanya naye kazi katika wimbo wake mpya.

Ali Kiba juzi alitambulisha wimbo wake mpya 'Dodo' huku Hamisa akiwa mpambaji wa video hiyo.

Akiileza hayo kwenye kipindi cha PlanetBongo cha East Africa Radio, Kiba amesema "Kufanya kazi na Hamisa Mobetto ni vizuri kwa sababu ana mashabiki wengi na kuhusu kuwa "video vixen" hata mimi nilikuwa sijui, kazi na idea hiyo imefanywa na timu yangu pamoja na uongozi wangu, hata mimi nilishangazwa sana kumkuta kule Zanzibar"



## Tattoo ya Billnass yamnogesha Nandy

RAPA Billnass, sasa yaonekana amenogewa na penzi la msanii mwenzake Nandy, kiasi ambacho ameamua kuchora mchoro wa tattoo kwenye mwili wake.

Amechora tattoo ya kwanza kwenye mwili wake, ambapo ameeleza kuwa imempatia maumivu makali.

Bila ya kutaja mchoro huo wa nani, kupitia posti yake aliyoweka katika mtandao wa Instagram, Billnass ameandika kwamba "Tattoo yangu ya kwanza, ni stori ndefu inauma sana, na nampenda yeye".

Baada ya kauli hiyo, mashabiki nao hawakutaka kuachwa nyuma na badala yake idadi kubwa walimuhoji aina ya mchoro au jina lake.

Kupitia mtandao wa Snapchat Nandy ambaye wana uhusiano wa kimapenzi, aliweka video fupi ambayo alimrekodi Billnass wakati anachora na kuandika, "Siwezi kuamini hili jina langu litakuwa kwenye mwili wake milele".

Video hiyo ya Nandy inathibitisha kuwa Billnass amechora tattoo ya jina la msanii huyo.



# 50 Cent kuibukia 'Black Mafia Family'

RAPA mkongwe kutoka Marekani, 50 Cent, anajaribu kurudi kivingine baada ya kutambulisha kipindi chake kipya kinachoitwa 'Black Mafia Family'.

50 Cent tayari amewashiwa taa ya kijani kuendelea na kazi hiyo ambayo inaweza kumpandisha tena baada ya kuporomoka kimuziki.

Kulingana na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Starz, Jeffrey Hirsch, kazi hiyo itafanyika kwa makubaliano kati yake na mwanamuziki huyo na faida itakayopatikana itanufaisha pande zote mbili.



## Kim kwa hilo unalolifanya Mungu anakuona

STAA wa mitindo, Kim Kardashian, ameendelea na utaratibu wake wa kuwasaidia watu waliofungwa Marekani, baada ya wiki hii kufanikiwa kumtoa jela jamaa mmoja.

Kim alifanikiwa kumuondolea adhabu David Jassy, ambaye amekaa gerezani miaka 11 wakati akitumikia adhabu yake ya kifungo cha miaka 15 jela.

Jassy kabla ya kupata msaada huo wa kisheria, alitiwa hatiana kwa kosa la kuua mtu na baada ya Kim kuajiri wanasheria kufuatilia kesi yake ikabainika hakuua kwa kukusudia.

## Card B eti 'amemisi' familia yake

MKALI wa hiphop kwa upande wa wanawake Marekani, Card B, amesema anaikumbuka familia yake baada ya nchi hiyo kuweka zuio la kutotoka nje kwa ajili ya kupambana na virusi vya corona.

Cardi B katika kipindi chote hawezi kufanya lolote ikiwa kukutana na mume wake baada ya nchi hiyo kutangaza amri hiyo.

Kulingana na Cable News Network (CNN), Marekani imeendelea kurekodi visa vya corona kufikia zaidi ya 399, 929 na vifo 12,911.





## Halima nakupa pongezi zako

MWIGIZAJI nyota wa Nollywood, Halima Abubakar, amejifungua mtoto wa kiume,

Halima miezi ya mwanzo mwaka jana alitangaza kuwa ana ujauzito na anatarajia kupata mtoto.

Katika ukurasa wake wa Instagram, mwigizaji huyo aliweka picha ya mikono ya mtoto wake huyo bila kuonyesha sura.

"Ni zawadi kutoka kwa Mungu, nakutakia maisha marefu," aliandika Halima.

## Drake kweli una mapenzi na Afrika

STAA wa muziki wa hiphop kutoka Canada, Drake, wiki hii amewashangaza mashabiki wake baada ya kumtaja mwanamuziki wa Nigeria, Rema, kwamba msanii mwenye kipaji cha kutisha.

Akitumia ukurasa wake wa Instagram, Dake alicheza muziki wa Rema na kuandika

"Upo juu Rema. Tuimbe pamoja nyimbo za kubembeleza."

Baada ya kuandika hayo aliendelea kucheza nyimbo hiyo na kusababisha mashabiki waliokuwa wakimfuatilia kumwagia pongezi.



MAKALA



# ‘LOCKDOWN’

# Zuio la kutotoka nje linaloleta mgawanyiko

Na Mwandishi Wetu

JANA ilikuwa Ijumaa kuu, siku ambayo ni mwanzo wa hatua mbalimbali za kusherehekea sikukuu ya Pasaka.

Katika sikukuu hii, waumini wa dini ya Kikristo, huwa na kawaida ya kujumuika katika makanisa mbalimbali kwa ajili ya kufanya ibada.

Katika mjumuiko huo, mshikamano, upendo na unyenyekevu unaonyeshwa na waumini, ikiwamo kutakiana heri kwa kuepeana mikono na kukumbatiana.

Lakini hilo halo haitashuhudiwa duniani kote katika kipindi hiki cha Pasaka, jamii nyingi zinajikuta zikiwa zinasherehekea zikiwa ndani ni ya nyumba zao, baada ya serikali za nchi nyingi kuweka zuio la kutotoka ndani katika kupambana na virusi vya COVID 19.

Kutokana na hali hiyo, wachambuzi na wataalam wa masuala ya kijamii wameelezea kuwa inaogopesha na inaweza kuleta athari chanya au hasi ndani ya familia.

Profesa Jacqui Gabb kutoka Chuo kikuu cha Open, anasema, imezoeleka katika kipindi kama hiki familia nyingi za nchi zilizoendelea zilikuwa na maandalizi mengi, lakini sasa hali ni tofauti.

Anasema wakati wa amri ya kutotoka majumbani ikiendelea, baba na mama wamejikuta wakikaa pamoja zaidi ya saa 15 au 16, huku wakiangalia watoto wao wanajisomea nyumbani.

Hali hii inafanya watu kuwa karibu zaidi tofauti na ilivyokuwa nyuma.

“Hatujawahi kupitia kipindi kama hiki,” anasema Profesa Gabb.

Familia kuwa pamoja kwa muda mrefu na kufanya shughuli zote pamoja huwa ni wakati wa sikukuu za Krismasi, kipindi ambacho watu wako likizo.

Lakini marufuku ya kutotembea nje ili kujikinga na maambukizi ya corona yamebadilisha mfumo wa maisha.

Familia wakiwa pamoja wakati wa sikukuu ya Krismasi,huwa wanapika pamoja na kufurahi pamoja, lakini sasa familia ziko pamoja zikiwa na hofu, msongo wa mawazo na huzuni.

Baadhi wamekuwa na hofu ya kupoteza ajira zao, fedha walizonazo haitoshi kujikimu na matunzo ya watoto inawaumiza vichwa zaidi.

“Mimi namlea mwanangu peke yangu, kipato changu ndicho tunakitegemea. Ninaweza kufanya kazi nyumbani lakini naona haiwezekani nikiwa na watoto wangu,” anasema Dk. Caroline Schuste.

Ninanapokaa muda mwingi bila kufanya kazi, ninaweza kupoteza ajira yangu.

“Mtoto wangu haendi shule na tunaishi na mama yangu mwenye miaka 84. Yani najiona sina namna, ukiwa ndani hakuna uhuru wa kufanya mambo yako,” anaongeza.

Wakati amri ya kutotembea na kukaa ndani ya nyumba ikitekelezwa, baadhi ya wataalamu wanahofia kuongezeka kwa vitebndo vya unyanyasaji wa kijinsia.

Hata hivyo kwa vijana hali imekuwa tofauti, wao wanaona marufuku hiyo inaongeza migogoro kati ya watoto na wazazi.

“Wazazi wangu wanaudhi. Nikishuka kwenye ngazi nawasalimia ‘habari ya asubuhi’ na wao huniambia ‘Mchana mwema’. Jambo hili ni sawa kuonekana mimi ni mvivu,” anasema Catherine John.

Amri ya kutotoka nje imekuwa ikionyesha mipaka kati ya walionacho na wale wasionacho, anaeleza Profesa Gabb. “Si rahisi kuweka video ya mazoezi na kujenga uhusiano kwa kila mtu ,” anaeleza.

Kauli yake inaungwa mkono na utafiti wa Shirika la Watoto la Save the Children, ambai unahofia kama wazazi na watoto wanapata chakula cha kutosha. Watoto pia wanapata hofu kuona mmoja wa familia yao akiugua corona, kupungua kwa chakula na kutoonana na marafiki

Mwalimu mmoja kutoka Hastings alituma ujumbe akiwaambia wazazi “kutojiumiza au kujihisi wakosaji” wakati wa siku hizi za kukaa ndani.

“Usijifanye kuwa shujaa,” aliwaambia. Alitoa ushauri kwamba kama hawawezi kudhibiti msongo wa mawazo, kuna njia nyingi ya kufanya ili kuwaweka sawa.

Mara watu wanaweza kuonesha kupenda kufanya mazoezi au kufanya usafi wa nyumba zao au bustani, kuwapa mtazamo kuwa wana nguvu ya kudhibiti.

“Haiwezekani kusimamia usomaji kwa njia ya mtandao kwa wanafunzi wa shule ya msingi na kufanya kazi kutokea nyumbani wakati huo huo,” aliandika Joseph Hellet.

Lakini Dokta Shah anapingana na mawazo hayo, yeye anasema hakuna ugumu katika kutekeleza vizuizi hivyo.

“Tusijiwekee wazo kuwa suala hili litakuwa gumu kwetu”, anasema.

Dokta Shah anasema bado hajafahamu watu wanatafuta nini ambacho kinaweza kuwa msaada wa kuwafanya wajisikie vizuri katika kipindi hiki.

Anaeleza inawezekana kuwa na suala la hofu na uchaguzi wa mavazi kutokana na hali ya kutotoka nje.

Dk. Shah hujisikia vizuri zaidi anapokuwa amevalia mavazi nadhifu ya kazini anapofanya kazi kutoka nyumbani.

Anasema haoni tofauti na huwa anashangaza watu pale wanapokuwa kwenye mkutano wa kikazi kwa kutumia video kupitia simu yake.

**Kwa msaada wa mitandao**

# Familia zijifunze uwekezaji wenye faida




Mkurugenzi wa Masoko na Uhusiano wa Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS, Daudi Mbaga (wa pili kulia), akitoa maelezo kwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, alipotembelea banda la UTT AMIS jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

MOJA ya mambo ambayo Watanzania wanashauriwa ni kuelekeza nguvu zao kwenye uwekezaji katika ngazi ya familia.

Uwekezaji ndani ya familia unaleta msaada na mabadiliko katika maisha yao ya sasa na baadaye.

Ushauri huo, umetolewa na Mkurugenzi wa Masoko na Uhusiano wa Mfuko wa Uwekezaji wa UTT- AMIS, Daudi Mbaga, wakati akifanya mahojiano maalum na gazeti hili.

**Kwa mfano ikiwekeza Sh. 200,000 kwa mwezi utakuwa umeweka milioni 24 kwa miaka 10, kama fedha hizo zitakuwa kwa riba ya asilimia 10 kwa mwaka utakuwa na milioni 40. 9," anasema.**

Mbaga anasema familia za Kiafrika zimekuwa pana tofauti na mataifa ya Ulaya, ndani ya nyumba moja kuna watu wasiopungua nane au zaidi.

Kitamaduni kwenye familia ya kiafrika mkuu wa kaya anawajibika kutekeleza matakwa ya watoto na wategemezi wengine, hata kama hayana msingi kwa maendeleo.

Miongoni mwa matakwa hayo kutaka vyakula vya gharama, badala ya kutumia vile vya kawaida ambavyo anavimudu kununua kwa bei nafuu.

Ulaji wa vyakula vinavyohitaji gharama kubwa kama baga, chipsi, mayai na kuku kila mara inaleta udumavu wa kiuchumi ndani ya familia.

Wazazi wanatakiwa kujipanga upya kwa kufanya uwekezaji mdogo kwa kutumia fedha kidogo walizonazo katika kujihakikishia maisha mazuri ya baadae.

"Familia nyingi hazina matumizi sahihi kulingana na mahitaji yao, mwisho wa siku kusababisha kuwa umaskini," anasema Mbaga.

"Unatakiwa kuchunga pesa zako, kumbuka kuna midomo mingi inahitaji lishe, pia kuna shida nyingine za maisha kama kununua mavazi, gharama za matibabu na malazi," anaongeza.

Mbaga anasema kama familia itakuwa na matumizi yanayolingana na kipato chao, kuna uwezekano mkubwa wakabakisha fedha na kuzifanyia uwekezaji.

Anaeleza moja ya uwekezaji ni pamoja na kununua vipande vya uwekezaji kupitia UTT-AMIS.

"Kwa mfano ikiwekeza Sh.200,000 kwa mwezi utakuwa umeweka milioni 24 kwa miaka 10, kama fedha hizo zitakuwa kwa riba ya asilimia 10 kwa mwaka utakuwa na milioni 40. 9," anasema.

Anafafanua kuwa kama riba ikiwa asilimia 12, uwekezaji wa mtu utakuwa milioni 46 ndani ya miaka 10, na kama uwekezaji huo ukiwa wa miaka 20, mhusika atakuwa na milioni 48. Kiasi hicho ukijumuisha asilimia 10, atakuwa na utajiri wa milioni 151.8.

Anasema, kipato chochote anachopata mtu ni lazima ajaribu kuweka kiasi hata kidogo kwa ajili ya dharura.

Amewakumbusha wazazi kwamba watoto wao wanahitaji kupata elimu, hivyo kupambana kwa njia hiyo ni jibu la kufanikisha malengo.

"Watu wanaokutegemea lazima waende kwa bajeti yako, na si kwa matamanio yao, wabane, waambie ukweli ili uweze kupata ziada kwa ajili ya uwekezaji wenye manufaa ya baadae," anasisitiza,

Aidha, anashauri kwamba wale wanaoweza kufanya kazi, watafute vibarua hata kwa wale wanaosubiri matokeo ya mitihani au waliopata likizo ili waongeze pato la familia.

"Jiulize kama watoto wako au ndugu wana madeni yametokana na nini? Je, kila mtu ana bima ya afya, maana maradhi yatakutoa kwenye malengo yako, fedha yote inaweza kuishia kwenye matibabu," anaeleza.

Anasema, katika maisha yaliyojaa malengo kuwapo na utaratibu wa kuwaeleza watoto ukweli kuhusu maisha. Mzazi akifanya hivyo, atakuwa umewapa watoto wake upendo wa kweli na kumnunulia si chipsi, mayai na kuku.

Anasema, bajeti inaweza kusababisha ugomvi katika familia kutokana na mahitaji ya kila siku kutowiana, lazima kuwapo mahitaji ya pamoja kuliko kila mtu kuwa hitaji lake binafsi.

Mke na mume wakipangilia fedha zao kwa pamoja na kuwekeza pamoja, fungu linakuwa kubwa na ni rahisi kumudu matumizi.

Vilevile fedha ikiwa nyingi, mtu anaweza kufanya jambo ambalo awali alikuwa huwezi kulifanya, miamala inakuwa rahisi na pia nguvu ya kujadili bei ya vitu vingine inaongezeka.

Jambo la muhimu ni familia kukaa pamoja kujadiliana kiungwana juu ya matumizi kwa pamoja na kukubaliana kuondoa tofauti.

Anaamini kwamba kushirikiana kwenye kila senti ni jambo gumu kwa wanandoa, kwa vile kila mmoja ana matumizi yake binafsi, lakini suala la kuwa na akaunti moja ni la msingi.

"Hakuna watu wawili wanafikiri sawa, na wana tabia sawa, hata mapacha hutofautiana, kila mtu aweke shida zake kando na fikra zenu ziende sawa, mjaribu kuwa na mtizamo mmoja," anasema Mbaga.

## HABARI KIMATAIFA

## Ulaya yatenga Euro Bil 500 kunusuru uchumi

**PARIS,** Ufaransa

WAWAKILISHI wa mataifa 19 wanaounda sarafu ya Euro, wamekubaliana kutolewa kiasi cha bilioni 500 kwa ajili ya kuuimarisha uchumi wa Ulaya.

Hatua hiyo, imefikiwa wakati nchi hizo zikipambana kunusuru kuanguka kwa uchumi kutokana na janga la corona.

Waziri wa fedha wa Ufaransa, Bruno La Maire, alisema makubaliano hayo ni hatua nzuri. Mataifa yenye uchumi mkubwa Ulaya, ambayo ni Ujerumani na Ufaransa yamekuwa yakipambana kupata suluhu dhidi ya athari za kiuchumi inayososababishwa ma janga hilo.

Waziri wa fedha wa Ujerumani ,Olaf Scholz, ameusifu uamuzi huo akitaja kama siku njema kwa mshikamano wa Ulaya.

Wakati huo huo, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, ameliomba baraza la usalama la Umoja huo kuonyesha mshikamano, wakati lilipokutana kujadiliana kuhusu janga la virusi vya corona.

Guterres alisema mbele ya baraza hilo lililogawanyika, kwamba mshikamano kati ya wanachama wake 15 utasaidia katika wakati huu wa mashaka.

Kikao hicho cha kwanza cha baraza hilo, kimefanyika kwa siri kupitia video, lakini Umoja wa Mataifa ulichapisha hotuba ya katibu mkuu. **DW**

## Masoko ya hisa yazidi kuimarika baada corona kupungua makali

**WASHINGTON,** Marekani

MASOKO ya hisa na mitaji duniani, yameimarika juzi kufuatia wawekezaji kutiwa moyo na taarifa zinazoonyesha kupungua kwa mlipuko wa virusi vya corona.

Soko la Hisa la Wall Street, limeshuhudia kupanda kwa kiwango cha mtaji, hatua inayoashiria kuwa wawekezaji wamepuuza tathmini za hivi karibuni zilizoonya kuwa uchumi wa dunia utadorora hadi kiwango cha chini kabisa mwaka 2020.

Masoko ya hisa ya kawaida ya Ulaya na Asia pia yaliimarika kwa sehemu fulani wakati biashara zilipofungwa siku ya Alhamisi.

Gavana wa Benki Kuu ya Marekani, Jerome Powell, amebashiri kuwa nchi hiyo itashuhudia kufufuka haraka kwa uchumi pindi virusi vya corona vitakapodhibitiwa.

Powell pia ametangaza mpango wa ukopeshaji wa kiasi cha dola trilioni 2.3, ili kuusaidia uchumi wa taifa hilo ambao ndiyo mkubwa zaidi duniani. **DW**

# Jiji la New York laelemewa wagonjwa wa corona

**NEW YORK,** Marekani

JIJI la New York limeorodhesha ongozeko la wagonjwa wa corona na kufanya liwe na idadi kubwa kuliko taifa lolote duniani.

Kulingana na takwimu mpya, serikali imethibitisha kwamba idadi ya watu walioambukizwa na virusi vya corona imeongezeka kutoka 10,000 siku ya Alhamisi hadi 159, 937.

Idadi hiyo ya wagonjwa inaiweka mbele ya Uhispania yenye 153,000 na Itali ilio na watu 143,000 wenye virusi hivyo.

China ambapo virusi hivyo vilianza mwaka uliopita iliripoti wagonjwa 82,000. Marekani imerekodi 462,000 na vifo vya watu 16,500.

**Katika Jimbo hilo la New York, watu 7000 wamefariki ikiwa nyuma ya Uhispania yemye vifo 15,500 na Itali imethinitisha watu 18,000.**

Takwimu hiyo inaonyesha duniani kuna takriban watu milioni 1.6 walioambikizwa na vifo 95,000.

Katika Jimbo hilo la New York, watu 7000 wamefariki ikiwa nyuma ya Uhispania yemye vifo 15,500 na Itali imethinitisha watu 18,000.

Picha zimeonekana za watu waliovalia magwanda ya kujikinga dhidi ya virusi vya corona wakiwazika watu walioifariki katika kaburi kubwa la pamoja mjini New York.

Picha zilizochukuliwa na kamera za juu, zilionyesha wafanyakazi wakitumia ngazi kuingia katika kaburi hilo kubwa ambapo majeneza hayo yalikuwa yamewekwa.

Picha hizo zilichukuliwa katika eneo la Hart Island kando ya mji wa Bronx , ambao umekuwa ukitumika kwa zaidi ya miaka 150 na maofisa wa baraza la mji kama eneo la makaburi ya pamoja.

Operesheni za mazishi katika eneo hilo zimeongezeka kutokana na mlipuko wa virusi, kutoka siku moja kwa wiki hadi siku tano kwa juma, kulingana na Idara ya magereza.

Wafungwa kutoka kisiwa cha Rikers ndio ambao wamekuwa wakifanyakazi hiyo, lakini ongezeko la kazi limefanya shughuli hiyo kuchukuliwa na manakandarasi.

Meya wa mji wa New York, Bill De Blasio, alisema mapema wiki hii kwamba, mazishi ya umma ya mji huo huenda yakatumika wakati wa mlipuko huu. **BBC**



Kiongozi wa kanisa la Katoliki duniani, Papa Francis, akiondoka kwenye alitare katika kanis la Mt. Peter Basilica Vatcan, bila kuwa na waumini baada ya kuwapo kwa amri ya kukaa majumbani katika kupambana na virusi vya COVID-19, nchini Italia. **PICHA: REUTERS**

# Baba wa Waziri Mkuu Uingereza ataka mwanawe apumzike

**LONDON,** Uingereza

WAZIRI Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson, ametoka kwenye chumba cha wagonjwa mahututi baada ya hali yake kuendelea kuimarika.

Hata hivyo, Johnson, bado anaendelea kubaki hospitali akiendelea na matibabu ya ugonjwa wa homa ya mapafu (Covid-19) unaotokana na maambukizi ya virusi vya corona.

Ofisi yake imeeleza kuwa waziri mkuu huyo anaendelea vyema.

Rais wa Marekani, Donald Trump, ametumia ukurasa wake wa Twitter kuelezea furaha yake kwa kiongozi huyo ambaye anamuita kuwa ni rafiki, kutoka katika chumba cha wagonjwa mahututi.

Kiongozi huyo alilazwa katika chumba cha wagonjwa mahututi kwa siku mbili baada ya hali yake kuzorota alipofikishwa hospitali.

Wiki iliyopita, aligunduliwa kuwa na dalili za wastani za ugonjwa huo na kujitenga nyumbani kwake huku akiendelea kuongoza shughuli za serikali.

Baba yake, Stanley Johnson, ameiambia BBC kuwa, mwanawe inambidi apumzike zaidi sasa baada ya kutoka kwenye chumba cha wagonjwa mahututi.

Mzee Johnson amesema hali ya mtoto wake imemfanya yeye binafsi awe makini zaidi na anaamini nchi yote imeliona hilo.

"Kuumwa kwake kumeifanya nchi nzima ione kuwa hili suala si la mzaha," alisema.

Ameongeza kuwa, kutakuwa na muda wa mpito kabla ya mtoto wake kurejea kazini kwa kuwa anahitaji kupumzika.

Katika kipindi ambacho Johnson amelazwa, Uingereza ipo chini ya uongozi wa kaimu waziri mkuu ambaye ni waziri wa mambo ya nje wa nchi hiyo Dominic Raab. **BBC**


# HADITHI

## Ananipwelepweta Penzi linalochanganya

NI kweli penzi halina macho, halina umri, rangi wala kabila. Penzi humea popote pale hata porini kama uyoga. Hata hivyo ni lazima kwanza kuna vitu vya kutazama kabla ya kuingia mzima mzima.

Tofauti isiyo ya kawaida ya umri ikizidi kwa wapendanao nalo ni tatizo. Lakini pia kuna umuhimu mkubwa ya kila mmoja kujua historia ya mwenzake wakati wa mapenzi, ili kama kuna shaka, basi kila mmoja anze uchunguzi, vinginevyo unaweza kujikuta umetumbukia kwenye penzi na ndugu yako.

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**




**Na Adam Fungamwango**

NI kweli penzi halina macho, halina umri, rangi wala kabila. Penzi humea popote pale hata porini kama uyoga. Hata hivyo ni lazima kwanza kuna vitu vya kutazama kabla ya kuingia mzima mzima.

Tofauti isiyo ya kawaida ya umri ikizidi kwa wapendanao nalo ni tatizo. Lakini pia kuna umuhimu mkubwa ya kila mmoja kujua historia ya mwenzake wakati wa mapenzi, ili kama kuna shaka, basi kila mmoja anze uchunguzi, vinginevyo unaweza kujikuta umetumbukia kwenye penzi na ndugu yako.

Hapa duniani kuna koo kubwa, mfano hapa Tanzania mtu anaweza kuwa na ndugu wa baba mkubwa au mdogo wakawa wanaishi mikoa mbalimbali, hivyo unaweza kukutana na mtu ukampenda kumbe ni mtoto wa baba yako mkubwa, mdogo, mama mkubwa au mdogo.

Hadi ndugu wajue hili, inawezekana kabisa mambo yakawa yameshaharibika.

**Mhagama akampigia simu baba yake kuwa mjini mambo yake ni poa, ana maisha mazuri, lakini pia ana mchumba anayetaka kumuoa.**

Haya yanatokea sana kwenye jamii yetu kwa sababu mbalimbali, ikiwamo kujulishana, kutopenda kufahamiana na hasa maisha ya sasa ambayo kila mtu kivyake na familia yake.

Kwenye filamu ya 'Ananipwelepweta' limetokea jambo kama hili la kuhuzunisha.

Mtunzi alikuwa anataka jamii ichukue tahadhari kabla hayajawakuta na wale yaliyowakuta, wawe mabalozi wazuri wa wenzao.

Imechezwa na wasanii wengi, lakini maarufu zaidi ni Riyama Ally na Slim Omari.

Imeanza kwa mzee Bungara na mkewe mama Somoe wakiishi kijijini maisha duni.

Ni maisha yaliyomchosha mama Somoe na kuamua kutoroka kijijini kwenda mjini kutafuta maisha.

Akamtoroka mumewe mzee Bungara, akiongozana na mtoto wake wa kike Somoe.

Kijijini alimuacha mumewe na mtoto wa kiume, Mhagama. Akiwa mjini aliomba vibarua kwa mama lishe na kulala njiani.

Kuna siku aligongwa na gari, lakini jamaa alikuwa msamaria mwema na kuamua kumpeleka hospitali, akimlipia pia matibabu hadi akapona.

Kama vile haitoshi, jamaa alimchukua na kumpeleka nyumbani kwake. Alimuuliza maswali ambayo baada ya kupata majibu yake na yeye akajitambulisha kuwa anaitwa Simba, naye alikimbiwa na mkewe na sasa anaishi peke yake. Mwisho wa yote akamtaka mama Somoe aishi pale kama mke.

Baada ya miaka kadhaa kupita, mama Somoe alibadilika na kutaka kurithi mali ya yote ya Simba na hakutaka kuwa mke tena. Akamuua na kurithi mali yote. Miaka 20 baadaye Mhagama alimuaga baba yake kuwa anakwenda mjini kutafuta kazi.

Aliingia mjini na kama kawaida hakuna kwenye wakati mzuri, kwani aliishia kusukuma mkokoteni wa maji.

Moja kati ya wateja wake ni mama Somoe. Shetani akamuingia mama wa watu. Akamtamani na kumfanya kibenteni. Jambo hili lilimkasirisha mno Somoe, lakini mama yake alitumia cheo cha umama kumyamazisha na kumtisha binti yake. Kazi ikawa ni kuponda raha na kula maraha, hadi mama wa watu kitumbo ndi.

Mhagama akampigia simu baba yake kuwa mjini mambo yake ni poa, ana maisha mazuri, lakini pia ana mchumba anayetaka kumuoa.

Mzee Bungara anamtuma jirani yake kijana Baraka aende mjini kwa mwanaye, lakini alipofika alishangaa kuona kwenye nyumba hiyo watu wote ndani anawafahamu.

Alishangaa kuona Mhagama akimtambulia mama Somoe kama mchumba wake, wakati anachofahamu ni mama yake mzazi. Mama Somoe naye anamtambua Baraka. Baraka anamwambia Mhagama kuwa mchumba 'ake ni mama yake mzazi, na yule binti yake ni Somoe ambaye ni mdogo wake. Mama anazirai. Anapelekwa hospitali na huko anafariki akiwa katika harakati za kujifungua kichanga cha mwanaye Mhagama.

**MWISHO**

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### ELIMU/ MASOMO

**REGISTRATION OPPORTUNITIES**

**KELAND NURSERY AND PRIMARY SCHOOL** located at salasala announces registration opportunities for Nursery and Primary School students. Call: 0713 327613.

### NYUMBA/VIWANJA

**NYUMBA INAUZWA,** Ninauza nyumba ya vyumba vinne vya kulala, kimoja ni master self contained. Ina vyumba vitano vya nyuma kimoja ni self contained, choo, bafu na jiko. Nyumba iko Ntyuka Dodoma karibu na shule ya sekondari Ntyuka. Nyumba iko kwenye kiwanja cha ukubwa wa SQM 2590. Ni nyumba nzuri sana kwa makazi na kupangisha. Kwa maelezo zaidi piga simu no. 0699-210258


***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu:


**IN THE DISTRICT DELEGATE OFDODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATIONCAUSE NO…2020**
**In the matter of the Estate of the LATE FRIDOLIN STEVEN MNONJELA OF MIYUJI DODMA CITY**
**And**
**In the matter of the Application for letters of Probate and Administration of estate by SHORAFIA ROMANUS GODIAT**

**CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules)**

All persons claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of Administration) is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before 13 of May 2020.

Dated at…this day of….2020

SHorafia
PETITIONER

Presented for filling this Day of April 2020

RESIDENT MAGISTRATE

DRAWN AND FILED BY: THE PETITIONER

156971

**TANGAZO**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya:**
**MOSHI MJINI**

**USIMAMIZI WA MIRATHI NO: 38 /2020**

Ombi la **ABDUL RAJABU KIMARO (2) ABDILAH R. KIMARO (3) RASHID R. KIMARO.**

Usimamizi wa mairathi ya marehemu RAJABU SELEMAN KIMARO

Kwa: YEYOTE ANAYEHUSIKA

Watu wote mnaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 16/4/2020. Kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 24/3/2020

115697002

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;98/2020**

Ombi la REHEMA NELSON MFUPA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu NELSON ISRAEL MFUPA

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 21/04/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 08/04/2020.

**TANGAZO LA KUPOTEA KWA OFFA YA KIWANJA**

**ABDALLAH MUSSA KAPANGA** AMBAYE NI MSIMAMIZI WA MIRATHI YA MUSSA KAPANGA MKAZI WA MJINI KATI MANISPAA YA SHINYANGA. ANATANGAZA KUPOTELEWA NA OFFA YA KIWANJA NAMBA 31KITALU "G" MJINI KATI MANISPAA YA SHINYANGA, AMBAYO ILIPOTEA MWAKA 2019 MAENEO YA SHINYANGA.

KWA YEYOTE ATAKAE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU AU AWASILIANE NA ABDALLAH MUSSA KAPANGA KWA SIMU NAMBA 0763385598.

**RB NAMBA SHY/RB/2020,**
**CONTROL NAMBA 991081234331 5.**


***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

**Nipashe**
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# MESSI AKATAA KUHUSISHWA INTER MILAN




**BARCELONA,** Hispania

NYOTA wa Barcelona, Lionel Messi, amekanusha taarifa za kuhusishwa na uhamisho wa kwenda Inter Milan na Newell's Old Boys na kuziita "habari za uongo."

Ripoti kutoka nchini Argentina, Hispania na Italia katika siku za hivi karibuni zimedai kwamba, Inter inaweza kutuma ofa ya kumsajili mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or, huku Barca ikidaiwa kuzungumza na Nerazzurri hao kuhusu mshambuliaji wao, Lautaro Martinez.

Taarifa hizo zimedai kwamba, mazungumzo yameshaanza na kwamba Martinez atatua pale Camp Nou na Messi kwenda Inter pamoja na nyota anayechipukia wa klabu ya Velez Sarsfield ya nchini Argentina, Thiago Almada.


Hata hivyo, Messi ameweka wazi kwamba hakuna ukweli wowote na habari hizo kwani ni uzushi tu.

Aliandika kwenye ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Instagram akisema: "Ni habari za uongo".

Alielezea habari za kuhusishwa na Inter ni "uongo namba moja" na pia alikanusha kuhusika kumlipia dhamana Ronaldinho, ambaye alitolewa jela wiki hiii.

Messi aliongeza: "Walisema pia kunihusisha na Newell's wiki chache zilizopita. Habari hizi ni za uzushi."

# Ballon d'Or kumwondoa Mane




**LIVERPOOL,** England

SADIO Mane anaweza kuhitaji kuondoka Liverpool ili kutimiza malengo yake ya kushinda tuzo ya Ballon d'Or, amesema mchezaji wa zamani wa kimataifa wa Senegal, Diomansy Kamara.

Fowadi huyo mwenye umri wa miaka 27 alimaliza katika nafasi ya nne kwenye tuzo hizo mwaka 2019, na wiki hii alibainisha kwamba anataka kuwa mwafrika wa pili kushinda tuzo hiyo baada ya George Weah.

Hata hivyo, mshambuliaji wa zamani wa Fulham, Leicester City na Celtic, Kamara amebainisha kuwa raia mwenzake huyo wa Senegal hawezi kutimiza ndoto zake akiwa pale kwenye dimba la Anfield.

"Kama Mane, siku moja anataka kushinda Ballon d'Or, anatakiwa kuondoka Liverpool kwa sababu kabu hiyo haiwezi kuwa bora kwake, licha ya kuwa katika kiwango cha kuvutia," amesema Kamara akinukuliwa na ESPN.

"Anahitaji kuwa kwenye klabu kubwa zaidi kama anataka kushinda tuzo hii na anaweza kuipata ndani ya miaka michache ijayo, kwani anastahili.

"Kwa sasa anahitaji kuendelea kupambana, na kubadilisha klabu, kwa sababu Liverpool haimpi Mane nafasi kubwa na watu wengi pake wanampigia kura Virgil van Dijk ingawa Mane yupo kwenye kiwango cha juu."

Van Dijk alimaliza nafasi ya pili nyuma ya mshindi Lionel Messi (686) lakini alikuwa mbele ya Cristiano Ronaldo (476), Mane (347) na Salah (178).

# Atletico, Sevilla zamwania Bellerin

**MADRID,** Hispania

KLABU za Atletico Madrid na Sevilla zinawania kumsajili Hector Bellerin wakati beki huyo wa pembeni wa Arsenal akihusishwa kutaka kurudi nyumbani Hispania baada ya kucheza kwa karibia miaka 10 jijini London.

Klabu hizo za Hispania zimeingia sokoni kwa ajili ya kutaka kumsajili beki huyo kipindi cha majira ya joto yanayokuja, wakitaka kuipiku Inter Milan ambayo inamwania pia nyota huyo mwenye umri wa miaka 25, kwa mujibu wa gazeti la Marca.

Bellerin, ambaye alijiunga na washikabunduki hao kutoka Barcelona mwaka 2011, amebakiwa na miaka mitatu kwenye mkataba wake wa sasa pale kwenye dimba la Emirates, maana yake klabu hizo zitatakiwa kulipa fedha ndefu ili kuipata saini yake.

Mchezaji huyo amecheza mechi 195 katika mashindano yote kwa klabu hiyo ya Ligi Kuu England, akifunga mabao nane na kutoa asisti 25.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka Hispania zimebainisha kwamba, Sevilla wanatafuta beki mpya wa kulia huku nyota wa zamani wa Manchester City, Jesus Navas, mwenye umri wa miaka 34 anayeonekana kuchoka, huku kijana Alejandro Pozo bado hajaaminiwa.

Wao Atletico Madrid kama wakifanikiwa kumsajili Bellerin maana yake atakwenda kupigania namba na Kieran Trippier aliyetua msimu huu pale kwenye dimba la Wanda Metropolitano.

Mchezaji huyo wa zamani wa Spurs alijiunga na kikosi hicho cha kocha, Diego Simeone kipindi cha majira ya joto kilichopita na amekuwa kwenye kikosi cha kwanza.



HABARI MICHEZO

# Mata amsifia Sancho akihusishwa kutua United

**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa Manchester United, Juan Mata, amemsifia Jadon Sancho "kama mchezaji mkubwa" wakati mshambuliaji huyo wa Borussia Dortmund akihusishwa kutakiwa na klabu hiyo.

Sancho mwenye umri wa miaka 20, amekuwa akihusishwa na miamba hao wa Ligi Kuu England baada ya kung'ara pale Dortmund kwa kipindi cha misimu miwili.

Akiwa kwenye mtandao wa Instagram Live, Mata aliulizwa kuhusu mchezaji huyo wa kimataifa wa England, ambaye ametajwa kwamba anawaniwa zaidi na United.

"Unataka mimi niseme nini?" alisema.

"Wote tunajua ni mchezaji mkubwa. Ana msimu wa kuvutia pale Borussia, lakini unajua sio jukumu langu kuzungumza mambo haya.

"Bila shaka nampenda kama mchezaji, lakini siwezi kujibu kuhusu hilo."

Sancho amefunga mabao 14 na kutoa pasi za mwisho 15 katika mechi 23 za Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, kabla msimu kusimamishwa kutokana na mlipuko wa corona.







# MULLER: NISINGESAINI MKATABA MPYA CHINI YA KOVAC

**MUNICH,** Ujerumani

THOMAS Muller anaamini kwamba, asingesaini mkataba mpya wa kuendelea kukaa pale Bayern Munich kama Niko Kovac angekuwa bado kocha wa timu hiyo.

Fowadi huyo wa zamani wa Ujerumani, Muller, mapema wiki hii amesaini mkataba mpya wa kuendelea kucheza hapo kwenye Uwanja wa Allianz Arena utakaomweka hadi Juni, 2023.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 kwa sasa anashika nafasi ya nne kwenye orodha ya wafungaji wa wakati wote wa Bayern akiwa amefunga mabao 195 katika mechi 521 alizocheza.

Hata hivyo, alijikuta kwenye wakati mgumu chini ya kocha, Kovac, ambaye alifukuzwa Novemba mwaka jana.

Tangu ujio wa Hansi Flick kama kocha wa muda, Muller amepata nafasi ya kucheza mara kwa mara, akifunga mabao sita na kutoa asisti 12 katika mechi 15 za Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

"Wakati wa majira ya kiangazi niliachwa kwenye kikosi cha kwanza katika mechi sita mfululizo. Ilikuwa wakati mgumu. Bila shaka, ikanifanya nifikiri," alisema katika mkutano na waandishi wa habari Alhamisi.

"Ulikuwa wakati mgumu kuelezea. Na naamini zingeweza kuongeza mkataba mpya katika hali ile.

"Baada ya kubadilishwa kwa kocha na kuanzisha staili tofauti ya uchezaji, mambo yamekuwa chanya zaidi."

# *Arteta apanga kusajili watatu*

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amesema Arsenal wanampango wa kusajili wachezaji wawili au watatu wakati wa dirisha la usajili, kabla ya kuanza msimu ujao.

Huku ligi za soka zikiwa zimesimamishwa kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa corona, Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), litaruhusu kubadilishwa kwa tarehe za usajili kama ligi zitachelewa kumaliza tofauti na ilivyopangwa.

Arteta amebainisha kwamba amejiandaa kwa namna tofauti katika usajili ujao na wataangalia namna soko litakavyokuwa.

Akizungumza na Sky Sports, kocha wa washikabunduki hao alisema: "Napanga kufanya usajili wa wachezaji wawili au watatu. Itategemea na mambo yatakavyokuwa.

"Hatujui bado mambo ya kifedha yatakuwaje, hatujui sheria na muda wa dirisha la usajili utakavyokuwa. Kuna vitu vingi ambavyo kwa sasa vipo nje ya uwezo wetu."

Arsenal ilitolewa kwenye Ligi ya Europa na Olympiacos Februari na ina nafasi finyu ya kufuzu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Washikabunduki hao walishinda mchezo mmoja tu kati ya nane Desemba mwaka jana, mwezi ambao Arteta alichukua mikoba kutoka kwa Unai Emery, lakini baadae wakashinda mechi nane na kutoka sare nne kati ya 13 kwenye mashindano yote tangu kuanza mwaka 2020.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# CHELSEA YAJITOSA KUMSAJILI CHILWELL

## ●●● Lengo ni kurithi mikoba ya Palmieri ambaye anawindwa na Juventus pamoja...

**LONDON,** England

MABOSI wa Chelsea wanajiandaa kumsajili beki wa kushoto wa Leicester, Ben Chilwell katika dirisha la usajili la majira ya joto litakapofunguliwa hivi karibuni.

**Chelsea inajipanga kuanza mchakato huo ili Chilwell arithi mikoba ya beki, Emerson Palmieri, ambaye anatarajia kuondoka na kujiunga ama Juventus au Napoli.**

Kocha Frank Lampard, anajiandaa kumnasa nyota huyo wa Timu ya Taifa ya England ili kumaliza tatizo ambalo timu yake ililipata katika msimu huu.

Marcos Alonso na Cesar Azpilicueta nyota hao wawili kwa pamoja na Emerson ambaye ana umri wa miaka 25 walishindwa kuonyesha kiwango kizuri na hivyo kukosa namba katika kikosi cha Lampard.

Endapo Juventus italipa dau la pauni milioni 25 lililotajwa ili kumsajili Emerson, itamfanya nyota huyo aungane na kocha wa zamani wa Chelsea Maurizio Sarri, ambaye bado ni shabiki wa Brazil, nchi aliyozaliwa licha ya kuwa ni raia wa Italia.

Naye Alonso anatajwa anajipanga kuondoka Stamford Bridge baada ya kutokuwa kwenye mipango ya kikosi cha Lampard chakutokana na kushindwa kung'ara kwenye nafasi yake.

Lakini inaelezwa kuwa kiungo huyo wa zamani wa klabu hiyo atatakiwa kupambana kuwania huduma ya Chilwell dhidi ya mabingwa watetezi wa Ligi Kuu England, Manchester City.

Chilwell amekuwa na namba ya kudumu katika kikosi cha kwanza cha England baada ya kuonyesha kiwango cha juu katika siku za hivi karibuni.

Foxes inatarajia kumuuza nyota huyo aliyekulia kwenye kituo chake cha vijana kwa dau la pauni milioni 50, ambaye pia amecheza mechi 118 tangu alipoanza kucheza kwenye timu A mwaka 2015.

## ZISIKUPITE

### MESSI AIKANA INTER

MSHAMBULIAJI wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Argentina, Lionel Messi (32), amekanusha taarifa za kuhusishwa na mpango wa kujiunga na Inter Milan, ameandika kwenye akaunti zake za mitandao ya kijamii. ***(Instagram)***

### ANCELOTTI KUMVUTA GREALISH

EVERTON inaamini kuendelea kufanya kazi chini ya Kocha Carlo Ancelotti kutasaidia mchakato wa kumsajili kiungo wa Aston Villa, Jack Grealish ambaye ana umri wa miaka 24, katika majira ya joto. ***(Football Insider)***

### LAMPARD ATAHADHARISHWA

BEKI wa zamani wa Chelsea, Frank Leboeuf amemwonya Kocha wa timu hiyo, Frank Lampard kuhusiana na uamuzi wake wa kutaka kumsajili kiungo wa Timu ya Taifa ya Brazil, Philippe Coutinho (27), ambaye anayeichezea Barcelona. ***(ESPN)***

### PEDRO AKARIBIA ROMA

ROMA imeonyesha nia ya kumsajili kiungo wa Chelsea, Pedro (32), ili kuhamia katika ligi hiyo ya Serie A, baada ya mkataba wa Mhispania huyo hapo Stamford Bridge kumalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Mirror)***

### CANCELO ANUKIA BARCA

BEKI wa Manchester City na Timu ya Taifa ya Ureno, Joao Cancelo (25), anawindwa na Barcelona katika mchakato ambao unaweza kumpeleka katika klabu hiyo ya England, Nelson Semedo (26). ***(Telegraph, subscription required)***

### MBAPPE APELEKWA MADRID

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Barcelona, Rivaldo (47), amemshauri mshambuliaji wa Paris St-Germain na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Kylian Mbappe kujiunga na Real Madrid mwishoni mwa msimu huu. ***(Betfair)***

### DOSU AMPONGEZA IGHALO

GOLIKIPA wa zamani wa Nigeria, Dosu Joseph amesema straika Odion Ighalo (30), amefanya vema kukamilisha mchakato wa kusaini mkataba wa kudumu wa kuitumikia Manchester United akitokea Shanghai Shenhua iliyomtoa kwa mkopo. ***(Goal.com)***

### SANCHEZ AIGOMEA UNITED

MANCHESTER United inapambana kusaka klabu itakayomnunua Alexis Sanchez (31), kwa sababu mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Chile, ambaye yuko kwa mkopo Inter Milan na amebakiza miaka miwili katika mkataba wake na klabu hiyo ya Old Trafford amekataa mshahara wake kupunguzwa. ***(Standard)***

### HAVERTZ AITAKA BAYERN

KIUNGO wa Bayer Leverkusen, Kai Havertz (21), amesema anataka kubakia Ujerumani na kujiunga na Bayern Munich mara dirisha la usajili la majira ya joto litakapofunguliwa.. ***(Sky Germany)***

### NAPOLI YAMTAKA ANDERSON

NAPOLI imeweka wazi nia yake ya kumsajili winga wa West Ham na Timu ya Taifa ya Brazil, Felipe Anderson, ambaye ana umri wa miaka 26. ***(Corriere dello Sport, in Italian)***

HABARI MICHEZO

## Madundo kuibeba Mwembeladu Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR.**

KOCHA Msaidizi wa Mwembeladu, inayoshiri Ligi ya Mkoa wa Mjini Magharibi (Kanda ya Unguja), Ramadhani Madundo, amesema mipango yake ni kuhakikisha timu hiyo inapanda daraja katika msimu ujao.

Madundo alisema aliamua kuondoka katika timu ya Ligi Kuu Zanzibar ya Chuoni na kurejea kuifundisha Mwembeladu kwa sababu anaamini kikosi hicho kitafikia malengo waliyonayo.

Kocha huyo alisema licha ya ugumu na ushindani uliopo, wachezaji wake wamejipanga kupambana ili lengo lao la kucheza Ligi Daraja la Kwanza litimie.

Alisema kusimamishwa kwa ligi mbalimbali kutokana na mlipuko wa virusi ya corona kumetibua mipango yake lakini anahakikisha wachezaji wanaendelea kufanya mazoezi kwa kutekeleza programu alizowapatia.

"Timu yetu inacheza vizuri licha ya ugumu wa ligi uliopo, timu zote zinaonyesha ushindani na kila timu inahitaji kupanda daraja , tukicheza vizuri zaidi kama tulivyoanza msimu, basi lengo letu litatimia," Madundo alisema.

Katika msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha klabu 18, Mwembeladu ipo kwenye nafasi ya pili.

## JKT Tanzania FC yapotezea usajili

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa JKT Tanzania, umesema unasubiri ripoti kutoka kwa Kocha Mkuu wa timu hiyo, Malale Hamsini, ili waanze maandalizi ya mchakato wa usajili wa wachezaji kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu Bara, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Uhusiano wa JKT Tanzania, Frank Lukwaro, alisema kwa sasa ni mapema kusema watasajili au wataacha wachezaji wangapi kwa sababu bado wanasubiri ripoti ya kiufundi ya Malale.

"Kuhusu usajili mpaka sasa hatujaanza mpaka tupate mapendekezo kutoka kwa kocha wetu, yeye ndiye amepewa madaraka ya kuamua tutafanya usajili wa aina gani," alisema Lukwaro.

Aliongeza wachezaji wao wote ambao mikataba yao inamalizika, watafanya nao mazungumzo kabla ya msimu huu haujamalizika.

"Katika kipindi hiki cha kujikinga na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona, benchi letu la ufundi lipo makini kuhakikisha kila mchezaji anafuata programu," Lukwaro alisema.

Aliongeza kocha wao ameahidi kikosi chake kitarudi uwanjani kikiwa na nguvu mpya kwa sababu wanahitaji kuhakikisha wanamaliza msimu kwa kufanya vizuri.

# MIRAJI AJIPANGA KUREJEA DIMBANI NA MOTO WAKE

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, Miraji Athuman, amesema mazoezi ya wiki mbili yatamfanya arejee katika ubora wake ule ule ambao alikuwa nao kabla ya kupata majeraha.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Miraji alisema anafanya mazoezi ya kunyonga baiskeli kwa ajili ya kujiweka sawa kabla ya kurudi rasmi uwanjani.

Miraji alisema mazoezi hayo ya wiki mbili yatamfanya arudi katika kiwango chake kilichozoeleka na lengo ni kusaidia Simba kutimiza malengo.

**"Nilipewa mazoezi ambayo naendelea kufanya ili kurejea kwenye ubora wangu, kwa muda wa wiki mbili nitakuwa ninaendesha kibaiskeli maalumu kwa ajili ya kujiweka sawa," alisema Miraji.**

Aliongeza mazoezi hayo yatamfanya awe kwenye nafasi na ubora wa juu kuliko hapo awali na baada ya kumaliza programu hiyo atasubiri maelekezo mengine kutoka kwa daktari wao.

"Ninamshukuru Mungu afya yangu imeimarika, nimefuata maelekezo yote niliyokuwa napewa na daktari wangu, ninajuwa mashabiki wangu wana kiu ya kuniona, nawaahidi nitarejea kwa kasi ile ile," Miraji alisema.

Miraji alipata majeraha ya mfupa mdogo katika mguu wa kulia ambayo aliyapata akiwa na timu ya Taifa (Taifa Stars), na baadaye alijitonesha majeraha hayo alipokuwa na klabu yake kwenye mchezo wa fainali wa Kombe la Mapinduzi dhidi ya Mtibwa Sugar ambapo Simba ilipoteza kwa kufungwa bao 1-0.

Simba ndio vinara wa Ligi Kuu Bara wakiwa na pointi 71 baada ya kushuka dimbani mara 28 na inahitaji pointi 12 ili itetee taji ambalo inalishikilia.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Uhuru Mchanganyiko, wakicheza mpira wa wavu katika Viwanja vya JMK Park jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**



# *Kagera: Maxime haendi kokote*

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kuwapo kwa tetesi za Yanga kuendelea kumwania Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, uongozi wa timu hiyo umesema kocha wake haendi kokote, imefahamika.

Inaelezwa kuwa Januari 15 mwaka huu, siku ambayo Yanga iliikaribisha Kagera Sugar katika mechi ya Ligi Kuu Bara, ilimpatia Maxime (pichani) nakala ya mkataba, ambao hadi kufikia jana nahodha huyo wa zamani wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), hajausaini.

Kiongozi mmoja wa juu wa Kagera Sugar aliliambia gazeti hili kuwa tayari wameshaboresha maslahi ya Maxime na wanaamini ataendelea kubakia katika klabu hiyo inayotumia Uwanja wa Kaitaba ulioko Bukoba, mkoani Kagera.

"Tunajua katika maisha kuna kuangalia maslahi, kwa kuzingatia hilo, tumeshauboresha mkataba wake wa awali na naweza kusema hata ofa ya Yanga ilikuwa haitofautiani sana na mshahara na bonasi anayolipwa hapa kwetu," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza Kagera Sugar imekuwa ikiwalipa vema wachezaji na waajiriwa wengine, hivyo uamuzi wa mtu kuondoka hautatokana na kigezo cha maslahi pekee.

Katika mchezo huo wa Januari 15, Kagera Sugar iliwachapa Yanga mabao 3-0, matokeo ambayo yaliendelea kuwatoa kwenye mbio za ubingwa.

Michezo
Jumamosi Aprili 11, 2020
Nipashe



Chelsea yajitosa kumsajili Chilwell UKURASA 30

# SILAHA MPYA KUTUA YANGA

●●● Ni mshambuliaji hatari kutoka UD Songo ya Msumbiji ambaye anatajwa...

**Na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha inatekeleza mapendekezo ya kukiimarisha kikosi chao kama ilivyopendekezwa na Kocha Mkuu wa Yanga, Luc Eymael (pichani), uongozi wa Yanga umeanza mchakato wa kunasa saini ya mshambuliaji, Jimmy Ukonde kutoka UD Songo ya Msumbiji.



**Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Mhamasishaji wa Yanga, Antonio Nugaz alisema uamuzi wa kumsajili Ukonde unatokana na ripoti ya benchi la ufundi la timu hiyo ambayo inahitaji kuimarisha safu hiyo ya ushambuliaji.**

Nugaz alisema mazungumzo kati Yanga na Ukonde yanaendelea vema na wanaamini asilimia 90 nyota huyo ambaye amewahi kucheza na winga wa Simba, Luis Miquissone atatua nchini kujiunga na klabu yao.

Alisema klabu imejipanga kukamilisha vema mchakato huo wa usajili kwa kushirikiana na wadhamini wao, Kampuni ya GSM ili malengo ya kutwaa ubingwa katika msimu ujao yatimie bila shaka.

"Baada ya viongozi na mdhamini GSM kukutana na kujadili mambo mbalimbali, ikiwamo suala la usajili, sasa macho yetu tunayaelekeza katika kumsajili, Jimmy Ukonde, ni kifaa ambacho kitakuja kuibeba Yanga, tunawaambia wajiandae, " alisema Nugaz.

Aliongeza kuwa Eymael ameridhishwa na kiwango cha Ukonde baada ya kumfuatilia kwenye mechi za hivi karibuni alizocheza akiwa na klabu yake.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, alisema pia klabu inaendelea na mazungumzo ya kuwaongezea mikataba wachezaji wao ambao mikataba yao ya awali inaelekea ukingoni na Eymael bado anahitaji huduma zao.

"Wakati tunaendelea na mipango ya kusaka wachezaji wapya, pia tunafanya mazungumzo na wachezaji wa zamani ambao kocha amependekeza tuwabakishe, nafasi kubwa tunayoipa kipaumbele ni ya ushambuliaji," Mwakalebela alisema.

Yanga pia inatajwa kuwinda saini ya nyota wawili kutoka Polisi Tanzania ambao ni kiungo, Baraka Majogoro na beki wa kati, Yassin Mustapha.

Hata hivyo wachezaji hao bado wana mikataba na timu hiyo inayomilikiwa na Jeshi la Polisi.



Beki wa Coastal Union, Bakari Mwamnyeto (kulia), akipambana kumdhibiti mshambuliaji wa Azam FC, Obrey Chirwa, katika mechi ya Ligi Kuu Bara hivi karibuni. **PICHA: MAKTABA**

## Kassim 'aiota' Simba ya 2003

**Na Somoe Ng'itu**

ALIYEKUWA Katibu Mkuu wa Simba, Kassim Dewji 'KD", ameweka wazi timu hiyo ilifanya vema katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwenye msimu wa 2003 kwa sababu walikuwa na kikosi bora kilichokuwa na wachezaji waliojitolea katika kiwango cha juu.

Msimu huo Simba ilitinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), kwa kuwaondoa waliokuwa mabingwa watetezi, Zamalek ya Misri.

Kassim aliliambia gazeti hili jana kuwa, Simba ilifanya vizuri katika michuano hiyo kwa sababu ya hatua za awali kupangwa na timu ndogo ambazo zilisaidia kuwajengea uzoefu wachezaji wao.

"Sisi tulianza katika utaratibu mdogo, sababu tulianza na timu za kawaida mno, tulikwenda Botswana tukashinda, tukacheza na Santos, tukasonga mbele kwa penalti hapa Dar es Salaam, tukapiga penalti 12, tukawatoa penalti 13 ndio tukawatoa," alisema Kassim.

Katibu huyo aliitaja mechi dhidi ya Zamalek ilikuwa na 'mitihani' kutokana na mazingira ya wakati huo lakini faida ya bao 1-0 waliloshinda katika mechi ya kwanza hapa nyumbani iliwaweka katika nafasi nzuri kwenye mchezo wa marudiano.

Alisema Simba ilikuwa na sehemu nzuri ya ufundi ambayo iliongozwa na marehemu Mkenya James Siang'a, na kupata ushirikiano kutoka kwa mako-cha wengine waliokuwa wanaishi Oman akiwamo, Talib Hilal.

"Kikosi kile kilikuwa ni kikosi madhubuti, siwezi kukisahau,...katikati nilikuwa na wigo mpana sana, nilikuwa na Gabriel (Emmanuel), Machupa (Athumani), Nteze (John), Mzee wa Kiminyio (Madaraka Selemani), lakini pia faida kubwa niliyokuwa nayo katika kiungo cha juu, nilikuwa na Yusuph Macho, Wilfred Keto, Shekhan Rashid, walikuwa viungo wengi sana, viungo wale walikuwa na uwezo wa kuisaidia timu kwenda mbele na kupata matokeo," Kassim alisema.

Aliongeza kuwa wachezaji wa sasa hawachezi kwa kujituma hali ambayo inasababisha timu kutolewa mapema kwenye michuano ya kimataifa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >